# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

آياتها ٤٠ سورة النبإ مكية (٧٨) (٨٠) ركوعاتها ٢

Ina Aya 40 — Ina Makkara 2

## SURATUN NABAA

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Wanaulizana habari gani?

عَمَّ يَتَسَاءَلُونَ ①

2. Ile habari iliyo kuu (ya kufufuliwa viumbe)

عَنِ النَّبَإِ الْعَظِيمِ ②

3. Ambayo wanakhitalifiana

الَّذِي هُمْ فِيهِ مُخْتَلِفُونَ ③

4. Nawakome! (Wasikhitalifiane). Hivi karibuni watajua (ukweli wake)

كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ④

5. Kisha nawakome! Hivi karibuni watajua (ukweli wake).

ثُمَّ كَلَّا سَيَعْلَمُونَ ⑤

6. Je! Hatukuifanya ardhi kuwa tandiko

أَلَمْ نَجْعَلِ الْأَرْضَ مِهَادًا ⑥

7. Na milima kuwa kama vigingi (vya ardhi)

وَالْجِبَالَ أَوْتَادًا ⑦

8. Na tukakuumbeni wanaume na wanawake

وَخَلَقْنَاكُمْ أَزْوَاجًا ⑧

9. Na Tukaufanya usingizi wenu kama kufa

وَجَعَلْنَا نَوْمَكُمْ سُبَاتًا ⑨

10. Na tukaufanya usiku kama guo (mnalofunikwa)

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ لِبَاسًا ⑩

11. Na tukaufanya mchana kama kufufuka.

وَجَعَلْنَا النَّهَارَ مَعَاشًا ⑪

الجزء الثلاثون (٣٠)

---

2. Habari kubwa ambayo makafiri walikuwa wakiulizana wenyewe kwa wenyewe, ni habari ya Utume wa Bwana wetu Muhammad (s.a.w.). Walikuwa wakiulizana: Ni kweli huyu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu? Na hili analodai kuwa Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu, na kuwa kuna siku ya Kiama, ni hakika mambo haya?

4. Tamko hili "*Kallaa*" limekuja mara kwa mara katika Qurani. Na mara huja kwa maana ya "Kukanya" (kukataza), na mara nyengine huja kwa maana ya "kukana" (kukanusha), na mara nyingine huja kwa maana ya "Kukokoteza" (kuthibitisha au kuhakikisha). Na kila mahali hufasiriwa kwa ifaavyo.

5. Mwenyezi Mungu anawaambia hapa kuwa wakome, wawache kudhani mambo ya batili Wakiwa hawajajua hata sasa kwamba Muhammad ni Mtume, na Mwenyezi Mungu ni Mmoja tu, na kuwa kuna Siku ya Mwisho ya kila mtu kulipwa kwa alilolitenda, basi hapo, yaani Siku ya Kiama, itawafunukia kweli, na watajua kwamba aliyokuwa akiwaambia Mtume ni ya kweli.

6. Tangu Aya hii mpaka Aya 16 Mwenyezi Mungu anawaonesha waja Wake neema nyingi alizowaneemesha, ili wafahamu kwamba, Mwenye kuneemesha neema kama hizi katika Ulimwengu, hawawachi waja Wake katika upotevu pasi na kuwaletea mtu wa kuwaongoa njia njema ya kuwafikisha katika neema za Dunia na Akhera, na kwamba Mwenye kufanya yote haya hapana jengine liwezalo kumshinda. Na maana ya "Tandiko" hapa ni mahali pa kumfaa mtu kufanya alitakalo katika maisha yake. Si mapendeleo yake kuwa Ardhi imekaa kama Tandiko la kitanda. (Taz. Sawi, katika Sura ya *Al-Ghashiyah*.)

12. Na tukajenga juu yenu (mbingu) saba madhubuti

وَبَنَيْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعًا شِدَادًا ﴿١٢﴾

13. Na tukaifanya taa ing'arayo na yenye joto kubwa

وَجَعَلْنَا سِرَاجًا وَهَّاجًا ﴿١٣﴾

14. Na tukateremsha maji yaangukayo kwa kasi kutoka mawinguni

وَأَنزَلْنَا مِنَ الْمُعْصِرَاتِ مَاءً ثَجَّاجًا ﴿١٤﴾

15. Ili kwayo Tuoteshe (vyakula vilivyo) chembe chembe na mimea (mengine)

لِّنُخْرِجَ بِهِ حَبًّا وَنَبَاتًا ﴿١٥﴾

16. Na mabustani yenye miti iliyosongana. (Basi Sisi tuliofanya yote haya itatushinda kufufua viumbe?)

وَجَنَّاتٍ أَلْفَافًا ﴿١٦﴾

17. Kwa hakika siku ya Hukumu imewekewa wakati maalumu

إِنَّ يَوْمَ الْفَصْلِ كَانَ مِيقَاتًا ﴿١٧﴾

18. Siku itakapopigwa parapanda (baragumu), nanyi mtafika makundi makundi

يَوْمَ يُنفَخُ فِي الصُّورِ فَتَأْتُونَ أَفْوَاجًا ﴿١٨﴾

19. Na mbingu zitafunguliwa ziwe milango milango

وَفُتِحَتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ أَبْوَابًا ﴿١٩﴾

20. Na milima itaondolewa na itakuwa kama mangati (mlenga) kama maji ukiona kwa mbali.

وَسُيِّرَتِ الْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا ﴿٢٠﴾

21. Kwa hakika Jahanamu inawangoja wabaya

إِنَّ جَهَنَّمَ كَانَتْ مِرْصَادًا ﴿٢١﴾

22. Ni makazi ya waasi

لِّلطَّاغِينَ مَآبًا ﴿٢٢﴾

23. Wakae humo dahari nyingi (karne baada ya karne).

لَّابِثِينَ فِيهَا أَحْقَابًا ﴿٢٣﴾

24. Hawataonja humo baridi (wala usingizi) wala kinywaji

لَّا يَذُوقُونَ فِيهَا بَرْدًا وَلَا شَرَابًا ﴿٢٤﴾

25. Ila maji yachemkayo sana na usaha

إِلَّا حَمِيمًا وَغَسَّاقًا ﴿٢٥﴾

26. (Wanalipwa) Malipo yaliyo sawa (na amali zao).

جَزَاءً وِفَاقًا ﴿٢٦﴾

27. Hakika wao hawakuwa wakiogopa hisabu (ya Mwenyezi Mungu)

إِنَّهُمْ كَانُوا لَا يَرْجُونَ حِسَابًا ﴿٢٧﴾

---

20. Yaani kama ambavyo mtu huona mlenge (mangati) akadhani ni maji, na hali hapana maji, kadhalika majabali Siku hiyo yataonekana yamethubutu kama yalivyokuwa, kumbe sivyo, yamekuwa kama pamba, yapeperushwa na upepo.

21. *Jahanamu* ni jina la moto maalumu huko Akhera. Mwenyezi Mungu anatupa Habari kwamba Jahanamu ni mahali pa kuwangojea makafiri ili walipwe humo malipo ya kukadhibisha kwao Mitume, baada ya kuwadhihirikia dalili za kuwa wao ni Mitume wa haki.

23. *Dahari* ni muda wa myaka mingi sana. Na muradi wa "dahari nyingi" ni kuwa watakaa milele katika Jahanamu kila ikiwapitia dahari itakuja dahari nyengine, na hivyo hivyo.

Katika Aya hii walioifanya ya 24 wameleta yale waliyoyaleta katika Aya ya 108 ya *Surat Hud;* na tumekwisha kujibu huko.

26. Yaani kama ambavyo hakuna madhambi makubwa kama ya ukafiri, kadhalika hakuna adhabu kubwa kama ya Jahanamu ndio iliyofanana na madhambi yao.

27. Mwenyezi Mungu anatuonesha kwamba sababu ya makafiri kufanya yote hayo ni kuwa wao hawaogopi kuhisabiwa Kesho Akhera, kwa sababu hawaamini Siku ya Hisabu. Na lau kama walikuwa wakiamini wangaliogopa, na wasingefanya mambo mabaya.

28. Na wakikadhibisha Aya Zetu kukadhibisha (kukubwa kabisa).

وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كِذَّابًا

29. Na (hali ya kuwa) kila kitu tumekidhibiti kwa kukiandika

وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ كِتَابًا

30. Basi onjeni (leo adhabu). Nasi Hatutakuzidishieni (kitu) ila adhabu (juu ya adhabu).

فَذُوقُوا فَلَن نَّزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا

31. Bila shaka wanaomcha Mwenyezi Mungu wamewekewa (mambo ya kuonyesha) kufuzu (kwao)

إِنَّ لِلْمُتَّقِينَ مَفَازًا

32. Mabustani na mizabibu

حَدَائِقَ وَأَعْنَابًا

33. Na wanawake vijana walio hirimu (na waume zao)

وَكَوَاعِبَ أَتْرَابًا

34. Na gilasi zilizojaa (vinywaji vizuri vizuri).

وَكَأْسًا دِهَاقًا

35. Hawatasikia humo (maneno ya) upuuzi wala ya kukadhibishana

لَّا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا كِذَّابًا

36. Watalipwa kutoka kwa Mola wako atia yenye kutosha

جَزَاءً مِّن رَّبِّكَ عَطَاءً حِسَابًا

37. Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake; Mwingi wa rehema; hawataweza kusema naye.

رَّبِّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الرَّحْمَٰنِ لَا يَمْلِكُونَ مِنْهُ خِطَابًا

38. Siku ambayo zitasimama Roho (za viumbe wote) na Malaika safu safu; hatasema siku hiyo ila yule ambaye (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa rehema amempa idhini (ya kusema) na atasema yaliyo sawa.

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أَذِنَ لَهُ الرَّحْمَٰنُ وَقَالَ صَوَابًا

39. Hiyo ndiyo Siku ya haki, (siku ya siku); basi anayetaka na ashike njia ende kwa Mola wake

ذَٰلِكَ الْيَوْمُ الْحَقُّ فَمَن شَاءَ اتَّخَذَ إِلَىٰ رَبِّهِ مَآبًا

40. Hakika Tunakuhadharisheni adhabu iliyo karibu (kufika), Siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake miwili; na kafiri atasema: "Laiti ningalikuwa udongo (nisipate adhabu hii inayoningoja sasa)"

إِنَّا أَنذَرْنَاكُمْ عَذَابًا قَرِيبًا يَوْمَ يَنظُرُ الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ وَيَقُولُ الْكَافِرُ يَا لَيْتَنِي كُنتُ تُرَابًا

---

36. Dini ya Uislamu inathubutisha raha mbili za Akhera: Raha ya Roho na raha ya kiwiliwili. Raha ya roho ni ya Radhi ya Mwenyezi Mungu Atakayowapa waja wake wema na yaliyo kama haya. Na raha ya kiwiliwili ni kama hii Aliyotaja hapa na katika Sura nyinginezo, kama mabustani ya kufurahisha macho, wanawake wazuri, vinywewa, vileo na kutosikia jambo la kuudhi na kama haya.

Angalia: Vileo vimekatazwa ulimwenguni kwa sababu ya madhara yake ambayo hayatapatikana katika vileo vya Akhera.

40. Dhahiri ya Qurani hapa, na wafasiri wote wanasema, kuwa adhabu iliyotajwa katika Aya hii waliyoifanya kuwa ya 41, ni adhabu itakayotokea Siku ya Kiama, si kama walivyosema wao hapa.

ايَاتُهَا ٤٦ (٧٩) سُوْرَةُ النّٰزِعٰتِ مَكِّيَّةٌ (٨١) رُكُوْعَاتُهَا ٢

Ina Aya 46 | **SURATUN NAZIAT** | Ina Makara 2

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

وَالنّٰزِعٰتِ غَرْقًا ①

1. Naapa kwa wale (Malaika) wavutao kwa nguvu (roho za watu wabaya)

وَّالنّٰشِطٰتِ نَشْطًا ②

2. Na kwa wale wanaotoa (roho za watu wema) kwa ulatifu (taratibu)

وَّالسّٰبِحٰتِ سَبْحًا ③

3. Na kwa wale wanaoogelea nazo (Wanaokwenda nazo mbio hizo roho)

فَالسّٰبِقٰتِ سَبْقًا ④

4. Wakazifikisha haraka huko wanakozifikisha

فَالْمُدَبِّرٰتِ اَمْرًا ⑤

5. Wakazitengezea mambo yake. (Mbaya zikaadhibiwa, na nzuri zikastareheshwa).

يَوْمَ تَرْجُفُ الرَّاجِفَةُ ⑥

6. (Mtafufuliwa) siku litakapolia baragumu la mwanzo (litakalotetemesha kila kitu).

تَتْبَعُهَا الرَّادِفَةُ ⑦

7. (Na) Lifuatiwe na baragumu la pili

قُلُوْبٌ يَّوْمَىِٕذٍ وَّاجِفَةٌ ⑧

8. Siku hiyo nyoyo zitapigapiga (kwa khofu)

اَبْصَارُهَا خَاشِعَةٌ ⑨

9. Macho yake yatainamia chini.

يَقُوْلُوْنَ ءَاِنَّا لَمَرْدُوْدُوْنَ فِى الْحَافِرَةِ ⑩

10. (Makafiri) wanasema (hapa duniani kwa stihizai): Je! Kweli tutarudishwa katika hali (yetu) ya kwanza? (Tutafufuliwa?)

ءَاِذَا كُنَّا عِظَامًا نَّخِرَةً ⑪

11. Hata tukiwa mifupa mibovu (iliyoliwa ndani)?

قَالُوْا تِلْكَ اِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ⑫

12. Wanasema (kwa stihizai): "Basi marejeo haya ni yenye hasara (kwetu)."

---

1-5. Katika Qurani mara nyingi Mwenyezi Mungu ameapa kwa viumbe Vyake, vilivyo na roho na visivyo kuwa na roho, vinavyoonekana na visivyoonekana. Na makusudio ni kutunabihisha tuzingatie hikima Yake katika kila kitu Alichokiapia ili tupate kujua Utukufu Wake na Uweza Wake Mkubwa. Na katika Sura hii Mwenyezi Mungu anaapa kwa Malaika wenye kazi za kutoa roho za makafiri kwa kuzivuta kwa nguvu, na wenye kutoa roho za Islamu kwa upole, na wenye kuogelea katika anga, na wenye kwenda mbio mbio na roho za watu wema Peponi, na za watu waovu Motoni, na wenye kudabiri mambo ayatakayo Mwenyezi Mungu.

8. Makusudio ya "nyoyo" hapa ni wenye nyoyo. Na muradi, Siku hiyo nyoyo za waovu zitatetemeka, na macho yao yatakodoka kwa sababu ya unyonge na khofu ya adhabu.

13. Kwa hakika hicho (Kiama) kitakuwa (kwa kupigwa) ukelele mmoja tu

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٣﴾

14. Mara wao (viumbe wote) watakuwa katika ardhi mpya.

فَإِذَا هُم بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾

15. Je! Imekufikia hadithi ya Musa?

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ مُوسَىٰ ﴿١٥﴾

16. Mola wake alipomwita katika bonde takatifu (liitwalo) Tuwaa.

إِذْ نَادَاهُ رَبُّهُ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٦﴾

17. (Akamwambia) Nenda kwa Firauni; hakika yeye amezidi (katika jeuri zake).

اذْهَبْ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَىٰ ﴿١٧﴾

18. Umwambie: Je, unapenda kujitakasa?

فَقُلْ هَل لَّكَ إِلَىٰ أَن تَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾

19. Nami nitakuongoza kwa Mola wako ili umche.

وَأَهْدِيَكَ إِلَىٰ رَبِّكَ فَتَخْشَىٰ ﴿١٩﴾

20. Basi alimuonesha Ishara kubwa kubwa, (miujiza mikubwa mikubwa).

فَأَرَاهُ الْآيَةَ الْكُبْرَىٰ ﴿٢٠﴾

21. Lakini alikadhibisha na akaasi.

فَكَذَّبَ وَعَصَىٰ ﴿٢١﴾

22. Kisha alirudi nyuma akaanza kufanya jitihadi (ya kuwazuilia watu wasimfuate Musa).

ثُمَّ أَدْبَرَ يَسْعَىٰ ﴿٢٢﴾

23. Basi aliwakusanya (watu) akanadi.

فَحَشَرَ فَنَادَىٰ ﴿٢٣﴾

24. Akasema: "Mimi ndiye mola wenu mkuu. (Huyo Mola wake Musa ni mdogo)".

فَقَالَ أَنَا رَبُّكُمُ الْأَعْلَىٰ ﴿٢٤﴾

25. Hapo Mwenyezi Mungu akamtia mkononi (akamtesa) kwa kulipa tamko lake hili la mwisho (la kusema kuwa yeye ndiye Mola mkubwa) na kwa lile tamko lake la mwanzo (alilosema kuwa hakuna Mola ila yeye tu).

فَأَخَذَهُ اللَّهُ نَكَالَ الْآخِرَةِ وَالْأُولَىٰ ﴿٢٥﴾

26. Kwa hakika katika haya limo onyo (kubwa) kwa wale wanaogopa.

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّمَن يَخْشَىٰ ﴿٢٦﴾

27. Je, nyinyi ni wenye umbo la nguvu zaidi au mbingu? Yeye amezijenga.

أَأَنتُمْ أَشَدُّ خَلْقًا أَمِ السَّمَاءُ ۚ بَنَاهَا ﴿٢٧﴾

28. Akainua kimo chake na Akazitengeneza vizuri

رَفَعَ سَمْكَهَا فَسَوَّاهَا ﴿٢٨﴾

---

15. Tangu Aya hii mpaka Aya ya 26 Mwenyezi Mungu anamliwaza Mtume Wake kwa kumtajia kisa cha Nabii Musa na namna alivyokadhibishwa na Firauni ili asione kuwa tabu hii imempata yeye peke yake, bali imeanza kuwafikilia ndugu zake, Mitume waliotangulia. Kadhalika katika Aya hizi muna utisho kwa makafiri ili wamuogope Mwenyezi Mungu Asije akawapatiliza kwa adhabu kama alivyompa tiliza Firauni na kaumu zake. Akawatosa baharini.

16. "Tuwaa" ni jina la hilo bonde ambalo Mwenyezi Mungu Alimlingana Nabii Musa Akampa Utume na kumuamrisha kwenda kwa Firauni.

27. Yaani Umbo lenu nyinyi ni la nguvu zaidi kuliko umbo la mbingu? hata mwone kwamba Mwenye Kuumba mbingu hawezi kukufufueni?

29. Na akautia giza usiku wake na akautokezesha mchana wake.

وَأَغْطَشَ لَيْلَهَا وَأَخْرَجَ ضُحَاهَا ﴿٢٩﴾

30. Na ardhi baada ya hayo Akaitandaza.

وَالْأَرْضَ بَعْدَ ذَٰلِكَ دَحَاهَا ﴿٣٠﴾

31. Akatoa ndani yake maji yake na malisho yake

أَخْرَجَ مِنْهَا مَاءَهَا وَمَرْعَاهَا ﴿٣١﴾

32. Na milima akaisimamisha

وَالْجِبَالَ أَرْسَاهَا ﴿٣٢﴾

33. (Kafanya haya yote) kwa ajili ya kukustarehesheni nyinyi na nyama wenu. (Basi aliyefanya yote haya si muweza wa kufufua?)

مَتَاعًا لَكُمْ وَلِأَنْعَامِكُمْ ﴿٣٣﴾

34. Basi itakapofika hiyo balaa kubwa (ya Kiama).

فَإِذَا جَاءَتِ الطَّامَّةُ الْكُبْرَىٰ ﴿٣٤﴾

35. Siku ambayo mtu atakumbuka kila alilolifanya

يَوْمَ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ مَا سَعَىٰ ﴿٣٥﴾

36. Na Moto mkali utaoneshwa kwa kila aonaye.

وَبُرِّزَتِ الْجَحِيمُ لِمَنْ يَرَىٰ ﴿٣٦﴾

37. Ama yule aliyeasi

فَأَمَّا مَنْ طَغَىٰ ﴿٣٧﴾

38. Na akapenda zaidi, (akayafadhilisha) maisha) ya dunia

وَآثَرَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٣٨﴾

39. Basi kwa hakika Jahanamu ndiyo itakayokuwa makazi yake.

فَإِنَّ الْجَحِيمَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿٣٩﴾

40. Na ama yule aliyeogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake, akaikataza nafsi yake na matamanio (maovu)

وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَى النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٤٠﴾

41. Basi (huyo) Peop ndiyo itakayokuwa makazi yake.

فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿٤١﴾

42. Wanakuuliza Kiama kutokea kwake kutakuwa lini?

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَاهَا ﴿٤٢﴾

43. Uko wapi na kuweza kutaja (wakati wa kuja Kiama)?

فِيمَ أَنْتَ مِنْ ذِكْرَاهَا ﴿٤٣﴾

44. Mwisho (wa ujuzi) wake uko kwa Mola wako.

إِلَىٰ رَبِّكَ مُنْتَهَاهَا ﴿٤٤﴾

45. Wewe ni Muonyaji (tu) kwa yule anayekiogopa.

إِنَّمَا أَنْتَ مُنْذِرُ مَنْ يَخْشَاهَا ﴿٤٥﴾

46. Siku watakapokiona watakuwa kama kwamba hawakukaa (ulimwenguni) ila jioni moja au mchana wake, (kwa kishindo, kitakachowafika).

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحَاهَا ﴿٤٦﴾ ع

---

33. Katika Aya hizi Mwenyezi Mungu anawaonesha kwamba Yeye ni Muweza wa mambo makubwa zaidi kuliko kufufua waliokufa, pamoja na kukumbusha Ukarimu Wake Mkubwa wa kutufanyia vitu vyote hivyo ili tunufaike.

46. Yaani wataona kuwa siku zote zilizowapitia ulimwenguni ni Kama kitambo kidogo tu.

اٰيَاتُهَا ٤٢ (٨٠) سُوْرَةُ عَبَسَ مَكِّيَّةٌ (٢٤) رُكُوْعُهَا ١

Ina Aya 42

## SURAT ABASA

Ina Kara 1

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Alikunja (Mtume) paji na akageuza uso

عَبَسَ وَتَوَلّٰىٓ ۙ ﴿١﴾

2. Kwa sababu alimjia kipofu.

اَنْ جَآءَهُ الْاَعْمٰى ۭ ﴿٢﴾

3. Na nini kilichokujulisha (ya kuwa huyo Sahaba pofu hahitaji mawaidha mapya)? Labda yeye atatakasika (kwa kusikia mawaidha mapya).

وَمَا يُدْرِيْكَ لَعَلَّهٗ يَزَّكّٰىٓ ۙ ﴿٣﴾

4. Au atakumbuka (aliyoyasahau); ukumbusho huo upate kumfaa

اَوْ يَذَّكَّرُ فَتَنْفَعَهُ الذِّكْرٰى ۭ ﴿٤﴾

5. Ama ajionaye hana haja (ya dini)

اَمَّا مَنِ اسْتَغْنٰى ۙ ﴿٥﴾

6. Wewe ndiye unayemshughulikia.

فَاَنْتَ لَهٗ تَصَدّٰى ۭ ﴿٦﴾

7. Na si juu yako kama hakutakasika.

وَمَا عَلَيْكَ اَلَّا يَزَّكّٰى ۭ ﴿٧﴾

8. Lakini anayekukimbilia

وَاَمَّا مَنْ جَآءَكَ يَسْعٰى ۙ ﴿٨﴾

9. Naye anaogopa

وَهُوَ يَخْشٰى ۙ ﴿٩﴾

10. Wewe unampuuza (Usifanye hivyo).

فَاَنْتَ عَنْهُ تَلَهّٰى ۚ ﴿١٠﴾

11. Sivyo! Hakika (Qurani) hii ni nasaha (mawaidha).

كَلَّآ اِنَّهَا تَذْكِرَةٌ ۚ ﴿١١﴾

12. Basi kila apendaye atawaidhika (asiyetaka basi — muachilie mbali)

فَمَنْ شَآءَ ذَكَرَهٗ ۘ ﴿١٢﴾ وقف لازم

13. (Mawaidha haya yanatoka) katika kurasa zilizohishimiwa

فِيْ صُحُفٍ مُّكَرَّمَةٍ ۙ ﴿١٣﴾

---

1. Siku moja Mtume (s.a.w.) alikuwa amekaa na wakubwa wa Maqureishi yu katika kuwalingania Dini, kwa hima kubwa, na akitaraji kuwa wakisilimu wao, na wanyonge wao watafuata; sababu wengi walijizuilia kwa kuwaogopa hao wakubwa wao. Wakati huo akatokea kipofu mmoja aitwaye Ibn-Ummi Maktum. Na pasi na kujua kuwa Mtume ameshughulika, akampigia ukelele. "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nifunze na mimi katika aliyokufunza Mwenyezi Mungu." Na akamkariria maneno haya. Mtume (s.a.w.) kwa kuwa alikuwa na pupa la kusilimu wale wakubwa, alimfinyia uso yule kipofu kwa kumuharibia kazi yake, wala asimsikize. Basi hapa Mwenyezi Mungu anamlaumu Mtume Wake kwa aliyoyafanya, ya kuwacha kumsikiza aliyemjia kutaka uongofu; kwa kutaraji kuamini watu wakubwa. Kwani huyo kipofu Mnyonge ni bora mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko hao wakubwa anaowataraji.

11-16. Hapa Mwenyezi Mungu, anamkataza Mtume wake asifanye tena kama hayo, na kumwambia kwamba Qurani ni Mawaidha, atakae kuzingatia atawaidhika, na asiyetaka hasara itamfikilia yeye. Na kumfahamisha kwamba Qurani ikatika Vitabu vitukufu (katika *Lauhil-Mahfudh)* vilivyo mikono ya Malaika Waandishi watukufu watenda mema, ambao ni bora kuliko Maqureishi.

| | |
|---|---|
| 14. Zilizotukuzwa, zilizotakaswa | مَّرْفُوعَةٍ مُّطَهَّرَةٍ ﴿١٤﴾ |
| 15. Zilizomo mikononi mwa (Malaika) waandishi (wa Mwenyezi Mungu) | بِأَيْدِي سَفَرَةٍ ﴿١٥﴾ |
| 16. Watukufu, Wacha Mungu. | كِرَامٍ بَرَرَةٍ ﴿١٦﴾ |
| 17. Ameangamia Binadamu namna gani ulivyo kwendelea mno ukafiri wake! | قُتِلَ الْإِنسَانُ مَا أَكْفَرَهُ ﴿١٧﴾ |
| 18. Kwa kitu gani Amemuumba? | مِنْ أَيِّ شَيْءٍ خَلَقَهُ ﴿١٨﴾ |
| 19. Kwa tone la manii; Amemuumba Akamuwęzesha (akampa uweza) | مِن نُّطْفَةٍ خَلَقَهُ فَقَدَّرَهُ ﴿١٩﴾ |
| 20. Kisha akamfanyia njia nyepesi (ya kufanya mambo yake) | ثُمَّ السَّبِيلَ يَسَّرَهُ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Kisha akamfisha na Akamueka kaburini | ثُمَّ أَمَاتَهُ فَأَقْبَرَهُ ﴿٢١﴾ |
| 22. Kisha Apendapo atamfufua. | ثُمَّ إِذَا شَاءَ أَنشَرَهُ ﴿٢٢﴾ |
| 23. La! Hajamaliza Aliyomuamuru (Mola wake). | كَلَّا لَمَّا يَقْضِ مَا أَمَرَهُ ﴿٢٣﴾ |
| 24. Hebu mwanaadamu naatazame chakula chake | فَلْيَنظُرِ الْإِنسَانُ إِلَىٰ طَعَامِهِ ﴿٢٤﴾ |
| 25. Hakika Sisi tumemimina maji kwa nguvu (kutoka mawinguni) | أَنَّا صَبَبْنَا الْمَاءَ صَبًّا ﴿٢٥﴾ |
| 26. Tena tukaipasuapasua ardhi | ثُمَّ شَقَقْنَا الْأَرْضَ شَقًّا ﴿٢٦﴾ |
| 27. Kisha Tukaotesha humo (vyakula vilivyo) chembe chembe | فَأَنبَتْنَا فِيهَا حَبًّا ﴿٢٧﴾ |
| 28. Na mizabibu na mboga | وَعِنَبًا وَقَضْبًا ﴿٢٨﴾ |
| 29. Na mizeituni na mitende | وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا ﴿٢٩﴾ |
| 30. Na mabustani, (mashamba) yenye miti iliyosongana barabara | وَحَدَائِقَ غُلْبًا ﴿٣٠﴾ |
| 31. Na matunda na malisho | وَفَاكِهَةً وَأَبًّا ﴿٣١﴾ |
| 32. Kwa ajili ya kukustareheshení nyinyi na wanyama wenu. | مَّتَاعًا لَّكُمْ وَلِأَنْعَامِكُمْ ﴿٣٢﴾ |
| 33. Basi itakapokuja sauti kali iumizayo mashikio, (sauti ya baragumu la Kiama) | فَإِذَا جَاءَتِ الصَّاخَّةُ ﴿٣٣﴾ |
| 34. Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye | يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿٣٤﴾ |

17. Hapa Mwenyezi Mungu anatuonesha ajabu ya mwanaadamu namna alivyokwendelea mno katika kufuru yake, kwa kuona kuwa Mwenyezi Mungu hataweza kumfufua baada ya kufa; pamoja na kuwa Yeye Ndiye aliyemuumba kwa tone la manii kisha akampitisha mahali pasipopitika, kisha akamlea hata akawa mtu wa kukamilika, kisha akamuua akamtia kaburini. Na atakapotaka atamfufua. Na hapana shaka kwamba kumzua mwanaadamu ni jambo kubwa zaidi kuliko kumrejeza katika hali aliyokuwa.

24. Ikiwa Mwanaadamu hakumbuki umbo la nafsi yake naatazame chakula akilacho namna kilivyopatikana, atafahamu uweza wa Mwenyezi Mungu.

35. Na mamaye na babaye — وَأُمِّهِۦ وَأَبِيهِ

36. Na mkewe na wanawe. — وَصَٰحِبَتِهِۦ وَبَنِيهِ

37. Kila mtu miongoni mwao Siku hiyo
atakuwa na hali itakayomtosha mwenyewe, (hana
haja ya mwenziwe.) — لِكُلِّ ٱمْرِئٍ مِّنْهُمْ يَوْمَئِذٍ شَأْنٌ يُغْنِيهِ

38. Siku hiyo nyuso nyingine zitanawiri — وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ

39. Zitacheka, zitachangamka. — ضَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ

40. Na nyuso nyingine Siku hiyo zitakuwa na
mavumbi juu yake — وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ عَلَيْهَا غَبَرَةٌ

41. Giza Totoro (kubwa) litazifunika. — تَرْهَقُهَا قَتَرَةٌ

42. Hao ndio makafiri watenda mabaya. — أُولَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْكَفَرَةُ ٱلْفَجَرَةُ

---

38,39. Siku hiyo wanaadamu watakuwa hali mbili: walioamini wakatenda amali njema, nyuso zao zitamemetuka kwa furaha, na waliokufuru wakatenda maovu, nyuso zao zitakuwa na vumbi na kupiga weusi, kama ilivyosema Aya za 40-42.

اٰيَاتُهَا ٢٩ (٨١) سُوْرَةُ التَّكْوِيْرِ مَكِّيَّةٌ (٧) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 29* **SURATUT TAKWYR** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Jua litakapokunjwakunjwa

إِذَا الشَّمْسُ كُوِّرَتْ ﴿١﴾

2. Na nyota zitakapopukutika

وَإِذَا النُّجُومُ انْكَدَرَتْ ﴿٢﴾

3. Na Milima itakapoendeshwa (angani kama vumbi)

وَإِذَا الْجِبَالُ سُيِّرَتْ ﴿٣﴾

4. Na ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa, (wasishughulikiwe)

وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ ﴿٤﴾

5. Na wanyama wa mwitu watakapokusanywa

وَإِذَا الْوُحُوشُ حُشِرَتْ ﴿٥﴾

6. Na bahari zitakapowashwa Moto

وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ﴿٦﴾

7. Na roho zitakapounganishwa (na viwiliwili vyake)

وَإِذَا النُّفُوسُ زُوِّجَتْ ﴿٧﴾

8. Na mtoto mwanamke aliyezikwa hali ya kuwa yuhai atakapoulizwa

وَإِذَا الْمَوْءُدَةُ سُئِلَتْ ﴿٨﴾

9. Kwa makosa gani aliuawa.

بِأَيِّ ذَنْبٍ قُتِلَتْ ﴿٩﴾

10. Na madaftari (ya amali) yatakapoenezwa (kila mtu akapewa lake)

وَإِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ ﴿١٠﴾

---

1. Sura nyingi zilizoshuka Makka zimetaja vituko vya Siku ya kiama: Na tangu Aya hii mpaka Aya 14 Mwenyezi Mungu ametaja baadhi ya vituko vya Siku hiyo.

1-13. Aya hizi walizozipa nambari hizi 2-14 wamezitilia farumu nyingi kabisa hata wamezigeuzia muradhi wa Mwenyezi Mungu alivyokusudia.

3. Siku hiyo majabali yatakuwa mepesi kama pamba inayoendeshwa na upepo.

4. "Ngamia wenye mimba" ni katika mali yaliyo bora mno kwa Waarabu, basi wanaambiwa hapa kwamba Siku hiyo watawatupilia mbali wasiwathamini tena.

5. Katika jumla ya vituko vya Siku hiyo ni nyama wa mwitu kukusanywa pamoja, nao wasidhuriane.

8-9. Aya mbili hizi zinaashiria hali waliyokuwa nayo Waarabu kabla ya kuja Uislamu, Mtu alikuwa akipata mtoto mwanamke humzika mzima, na wakisema kwamba vijana wanawake hawana faida, bali ni hasara tupu; ya kumlea na kumlisha na kumvisha, na akiharibika itakuwa aibu juu ya wazee wake na jamaa zake wote. Ilipokuja Dini ya Uislamu ikakataza munkari huu. Na hapa Mwenyezi Mungu anatuonesha kwamba Siku hiyo, yule mtoto aliyezikwa mzima ataulizwa ameuliwa kwa makosa gani? Naye atajibu kwamba hakufanya makosa yoyote, bali ameuliwa kwa dhulma tu.

10. Hayo ni madaftari ya hisabu yaliyodhibiti mema ya mtu na maovu yake. Siku hiyo kila mtu atapewa yake, aone mwenyewe mema yake na maovu yake.

| | |
|---|---|
| 11. Na utando wa mbingu utakapotanduliwa | وَإِذَا السَّمَاءُ كُشِطَتْ ۝١١ |
| 12. Na Jahanamu itakapochochewa | وَإِذَا الْجَحِيمُ سُعِّرَتْ ۝١٢ |
| 13. Na Pepo itakaposogezwa | وَإِذَا الْجَنَّةُ أُزْلِفَتْ ۝١٣ |
| 14. (Wakati huo) kila nafsi itajua ilichokihudhurisha, (amali ilizofanya). | عَلِمَتْ نَفْسٌ مَّا أَحْضَرَتْ ۝١٤ |
| 15. Basi Naapa kwa nyota zinazorejea nyuma | فَلَا أُقْسِمُ بِالْخُنَّسِ ۝١٥ |
| 16. Zinazokwenda, kisha zikajificha | الْجَوَارِ الْكُنَّسِ ۝١٦ |
| 17. Na kwa usiku uingiapo | وَاللَّيْلِ إِذَا عَسْعَسَ ۝١٧ |
| 18. Na kwa asubuhi inapopambazuka | وَالصُّبْحِ إِذَا تَنَفَّسَ ۝١٨ |
| 19. Kwa hakika hii (Qurani) ni kauli (aliyokuja nayo) Mjumbe mtukufu (Jibrili) | إِنَّهُ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ۝١٩ |
| 20. Mwenye nguvu, mwenye cheo cha hishima kwa Mwenyezi Mungu | ذِي قُوَّةٍ عِندَ ذِي الْعَرْشِ مَكِينٍ ۝٢٠ |
| 21. Anayetiiwa huko (mbinguni na Malaika wenziwe), kisha muaminifu. | مُّطَاعٍ ثَمَّ أَمِينٍ ۝٢١ |
| 22. Na kuwa mwenzenu (huyu Muhammad) si mwendawazimu (kama mnavyomsingizia). | وَمَا صَاحِبُكُم بِمَجْنُونٍ ۝٢٢ |
| 23. Na hakika yeye alimuona (Jibrili) katika upeo wa macho (mbinguni) ulio safi. | وَلَقَدْ رَآهُ بِالْأُفُقِ الْمُبِينِ ۝٢٣ |

---

12-13. Siku hiyo Pepo watakurubishiwa watenda mema, na Moto watakurubishiwa watenda maovu, kila mmoja aone mahali pake.

14. Kila mtu Siku hiyo atajua amali aliyoitenda ikiwa njema au mbaya. Ataziona katika daftari yake.

15-16. Kuna nyota ambazo huenda pamoja na Jua na Mwezi, kisha zikarejea zilokako, na kujificha chini ya muangaza wa jua. Nazo ni hizi tano: Utarid (Mercury), Zuhra (Venus), Mirrikh (Mars), Mushtary (Jupiter) na Zuhal (Saturn).

19-21. Mjumbe Mtukufu na mwenye kutiiwa huko mbinguni ni Jibrili, ambaye ndiye mkubwa wa Malaika wote. Na yeye ndiye aliyekuwa akichukuwa Qurani kwa amri ya Mwenyezi Mungu akimletea Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu amemsifu Jibrili kwa sifa hizi, ili kutuonesha utukufu wa Qurani na utukufu wa Mtume (s.a.w.); sababu mtu mtukufu hupelekewa mjumbe mtukufu, na amana bora hupewa mjumbe bora.

22-25. Makafiri walipokuwa hawana tena la kusema, wala hoja ya kumtolea Mtume (s.a.w.); walikuwa wakitoa khabari za uwongo kuwe Mtume ana wazimu, wala maneno hayo hakupewa na Jibrili, wala hakumuona kamwe, bali alimuona Shetani, na hayo ayasemayo ni maneno ya Shetani tu. Basi Mwenyezi Mungu anawarudi kwa Aya hizi.

23. Yaani Mtume alimuona Jibrili katika pambizo za mbingu.

24. Hapa pana viraa viwili: (a) "dhanin" (kwa dhwee). Na maana yake ni mwenye kutuhumiwa. Na muradi wake ni kuwa Mtume (s.a.w.) si wakutiliwa shaka kwa lolote alitolealo khabari; hapana shaka kuwa ni kweli tu. (b) "dhanin" (kwa dhwad). Na maana yake ni bakhili, na muradi wake ni kuwa Mtume hafichi wala hapunguzi kitu katika mambo aliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu kuyafikisha kwa waja Wake.

24. Wala yeye si bakhili wa (kukuelezeni) mambo ya ghaibu.

وَمَا هُوَ عَلَى الْغَيْبِ بِضَنِينٍ ﴿٢٤﴾

25. Wala hii si kauli ya Shetani aliyefukuzwa (katika rehma ya Mwenyezi Mungu)

وَمَا هُوَ بِقَوْلِ شَيْطٰنٍ رَّجِيمٍ ﴿٢٥﴾

26. Basi mnakwenda wapi?

فَأَيْنَ تَذْهَبُونَ ﴿٢٦﴾

27. Haikuwa hii Qurani ila ni ukumbusho kwa walimwengu wote

إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِّلْعٰلَمِينَ ﴿٢٧﴾

28. Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kushika njia.

لِمَن شَآءَ مِنكُمْ أَن يَسْتَقِيمَ ﴿٢٨﴾

29. Wala nyinyi hamtataka isipokuwa atake Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu wote.

وَمَا تَشَآءُونَ إِلَّآ أَن يَشَآءَ اللّٰهُ رَبُّ الْعٰلَمِينَ ﴿٢٩﴾ ع

---

29. Mtu hawezi kuongoka, ila kwanza atake mwenyewe kuongoka; na hayo matakwa na uweza wa kufanya kheri na shari, na kuwacha, amepewa na Mwenyezi Mungu. Amemuumbia Yeye Mwenyezi Mungu.

اٰياتها ١٩ (٨٢) سورة الانفطار مكية (٨٢) ركوعها ١

*Ina Aya 19* **SURATUL INFITAR** *Ina Karu 1*

*(Imeteremka Makka)*

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.**

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Mbingu zitakapo pasuka

إذا السماء انفطرت ۝١

2. Na nyota zitakapo pukutika

وإذا الكواكب انتثرت ۝٢

3. Na bahari zitakapopasuliwa

وإذا البحار فجرت ۝٣

4. Na makaburi yatakapofukuliwa

وإذا القبور بعثرت ۝٤

5. (Kila) nafsi (wakati huo) itajua iliyoyatanguliza na iliyoyabakisha nyuma.

علمت نفس ما قدمت وأخرت ۝٥

6. Ee mwanaadamu! Ni nini kikudanganyacho na Mola wako Mtukufu (hata ukamuasi)

يا أيها الإنسان ما غرك بربك الكريم ۝٦

7. Aliyekuumba na kukutengeneza, kisha akakulinganisha sawa?

الذي خلقك فسواك فعدلك ۝٧

8. Katika sura yoyote Aliyoipenda Amekutengeneza.

في أي صورة ما شاء ركبك ۝٨

9. Sivyo hivyo! Bali nyinyi mnaikadhibisha (siku ya) Malipo.

كلا بل تكذبون بالدين ۝٩

10. Na hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza

وإن عليكم لحافظين ۝١٠

11. Watukufu wenye kuandika

كراما كاتبين ۝١١

12. Wanayajua yote mnayoyatenda (na wanadhibiti).

يعلمون ما تفعلون ۝١٢

---

1. Tangu Aya ya 1-4 Mwenyezi Mungu Atuonesha vituko vyengine vya Siku ya Kiama.

5. Kila mtu Siku hiyo atajua alichokifanya na alichokiwacha katika amali njema na mbaya.

6-7. Maana ni lipi lililokuhadaa hata ukamuasi Mola wako Mtukufu Aliyekuumba, akakukamilisha, Akakulinganisha? Mwenyezi Mungu baada ya Kumuumba mwanaadamu Amemkamilisha umbo lake kwa kumtia kila kiungo akihitajiacho, hata lau kama chapungua kimoja, asingeweza kutekeleza haja zake. Kisha amemlinganisha kwa kukifanya kila kiungo ni mnasaba wa kiwiliwili chake, asifanye viungo vyake ni virefu au vifupi kuliko kiasi au . . .

9. Hapana lililokuhadaa isipokuwa kutoamini na kukadhibisha Siku ya kila mtu kujaziwa kwa amali zake.

10. Kila mtu ana Malaika wawili: "Rakib" na "Atid." Na kazi zao ni kuandika mema ya mtu na maovu yake. Ndio muradi wa "Wenye kuwatunza, Watukufu, wenye kuandika."

13. Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani

إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿١٣﴾

14. Na waovu watakuwa Motoni.

وَإِنَّ الْفُجَّارَ لَفِي جَحِيمٍ ﴿١٤﴾

15. Wataingia humo siku ya Malipo.

يَصْلَوْنَهَا يَوْمَ الدِّينِ ﴿١٥﴾

16. Wala hawatatoka humo.

وَمَا هُمْ عَنْهَا بِغَائِبِينَ ﴿١٦﴾

17. Na nini kitakachokujulisha siku ya Malipo ni siku gani hiyo!

وَمَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمُ الدِّينِ ﴿١٧﴾

18. Tena nini kitakachokujulisha siku ya Malipo ni siku gani hiyo!

ثُمَّ مَا أَدْرَاكَ مَا يَوْمُ الدِّينِ ﴿١٨﴾

19. Ni Siku ambayo nafsi haitaimilikia nafsi (nyingine) cho chote; na amri siku hiyo itakuwa ya Mwenyezi Mungu (tu).

يَوْمَ لَا تَمْلِكُ نَفْسٌ لِنَفْسٍ شَيْئًا وَالْأَمْرُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ ﴿١٩﴾

---

16. Mapendeleo "si wenye kuepukana nao."

17. Maana ni lipi la kukufahamisha hata uijuwe Siku ya malipo ni ipi? Maneno ya namna hii hutumia Waarabu katika kulitukuza jambo na kulitilia kitisho.

19. Yaani Siku ambayo hapana mtu atakayeweza kumfaa mwenziwe kwa lolote, wala hakuna atakayekuwa na uweza wa lolote au kutoa amri yoyote isipokuwa Mwenyezi Mungu Peke yake.

اٰيَاتُهَا ٣٦ (٨٣) سُوْرَةُ الْمُطَفِّفِيْنَ مَكِّيَّةٌ (٨٦) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 36* — *Ina Kara 1*

## SURATUL MUTAFFIFYN

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Maangamizo yatawathubutikia wapunjao (wenziwao)

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِيْنَ ۙ ١

2. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili

الَّذِيْنَ اِذَا اكْتَالُوْا عَلَى النَّاسِ يَسْتَوْفُوْنَ ۖ ٢

3. Lakini wanapowapimia kwa (kipimo cha) vibaba au mizani (au vinginevyo), wao hupunguza.

وَاِذَا كَالُوْهُمْ اَوْ وَّزَنُوْهُمْ يُخْسِرُوْنَ ۗ ٣

4. Je! Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa

اَلَا يَظُنُّ اُولٰٓئِكَ اَنَّهُمْ مَّبْعُوْثُوْنَ ۙ ٤

5. Katika Siku iliyo kuu

لِيَوْمٍ عَظِيْمٍ ۙ ٥

6. Siku watakaposimama watu (wote) mbele ya Mola wa walimwengu wote?

يَّوْمَ يَقُوْمُ النَّاسُ لِرَبِّ الْعٰلَمِيْنَ ۗ ٦

7. Sivyo hivyo (mnavyofanya)! Kwa hakika maandishi (ya amali) za waovu yamo katika Sijjin—

كَلَّآ اِنَّ كِتٰبَ الْفُجَّارِ لَفِيْ سِجِّيْنٍ ۗ ٧

8. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ujue hiyo) sijjin ni kitu gani?

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا سِجِّيْنٌ ۗ ٨

9. Ni daftari lililoandikwa (ndani yake amali za watu wabaya).

كِتٰبٌ مَّرْقُوْمٌ ۗ ٩

10. Adhabu kali siku hiyo itawathubutikia wanaokadhibisha

وَيْلٌ يَّوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِيْنَ ۙ ١٠

11. Ambao wanaikadhibisha Siku ya Malipo.

الَّذِيْنَ يُكَذِّبُوْنَ بِيَوْمِ الدِّيْنِ ۗ ١١

12. Wala haikadhibishi ila kila mwenye kuruka mipaka, mwenye dhambi; (anajitia pambani kusudi za kujidai kuikadhibisha)

وَمَا يُكَذِّبُ بِهٖٓ اِلَّا كُلُّ مُعْتَدٍ اَثِيْمٍ ۙ ١٢

13. Anaposomewa Aya Zetu husema: "Ni visa vya watu wa kale."

اِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِ اٰيٰتُنَا قَالَ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ ۗ ١٣

---

7. Baada ya Madaftari ambayo kila mtu atapewa lake akhera aone amali zake njema au mbaya, kuna na Madaftari mengine makubwa: moja limedhibiti amali za watu wabaya wote, ndilo "Sijjin" na moja limedhibiti amali za watu wema wote ndilo "Illiyyin" itakayo tajwa katika Aya ya 18 ya sura hii hii.

10. Kukadhibisha ni namna tatu: (a) Kukadhibisha kwa maneno na vitendo; (b) Kukadhibisha kwa vitendo tu, kama kuambiwa kuwa jambo kadha ni baya, na mtu akajua kuwa kweli ni baya na akalitenda lile lile pasi na kujali; na (c) Kukadhibisha kwa maneno tu; nako ni kama mtu kujua jambo kadha ni haramu, na juu ya hivi akasema ni halali.

14. Sivyo hivyo! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao (maovu) waliyokuwa wakiyachuma.

كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَىٰ قُلُوبِهِم مَّا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١٤﴾

15. Sivyo hivyo! Hakika watazuiliwa, siku hiyo na (neema za) Mola wao.

كَلَّا إِنَّهُمْ عَن رَّبِّهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّمَحْجُوبُونَ ﴿١٥﴾

16. Kisha wataingia katika Moto (uwakao).

ثُمَّ إِنَّهُمْ لَصَالُو الْجَحِيمِ ﴿١٦﴾

17. Kisha waambiwe: "Haya ndiyo mliyokuwa mkiyakadhibisha".

ثُمَّ يُقَالُ هَٰذَا الَّذِي كُنتُم بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿١٧﴾

18. Sivyo hivyo (mnavyofanya: Wacheni mabaya!) Hakika Maandishi ya (amali za) watu wema yamo katika (daftari linaloitwa) Iliyyin_

كَلَّا إِنَّ كِتَابَ الْأَبْرَارِ لَفِي عِلِّيِّينَ ﴿١٨﴾

19. Na ni jambo gani litakalo kujulisha hata uijue hiyo (Illiyyin) ni kitu gani_

وَمَا أَدْرَاكَ مَا عِلِّيُّونَ ﴿١٩﴾

20. (Hilo) ni daftari ambalo zinaandikwa humo (amali za watu wazuri)

كِتَابٌ مَّرْقُومٌ ﴿٢٠﴾

21. Wanaliona wale waliokaribishwa (na Mwenyezi Mungu).

يَشْهَدُهُ الْمُقَرَّبُونَ ﴿٢١﴾

22. Kwa hakika wafanyao wema watakuwa neemani

إِنَّ الْأَبْرَارَ لَفِي نَعِيمٍ ﴿٢٢﴾

23. Wakae juu ya viti vya fakhari wakitazama (starehe zao)

عَلَى الْأَرَائِكِ يَنظُرُونَ ﴿٢٣﴾

24. Utaona alama za neema katika nyuso zao.

تَعْرِفُ فِي وُجُوهِهِمْ نَضْرَةَ النَّعِيمِ ﴿٢٤﴾

25. Watanyweshwa vinywaji (vizuri) vilivyofungwa (kwa vizibo madhubuti)

يُسْقَوْنَ مِن رَّحِيقٍ مَّخْتُومٍ ﴿٢٥﴾

26. Mwisho wake (vinwaji hivyo vinaleta harufu ya) miski. Na katika (kupata) haya washindane wenye kushindana_

خِتَامُهُ مِسْكٌ وَفِي ذَٰلِكَ فَلْيَتَنَافَسِ الْمُتَنَافِسُونَ ﴿٢٦﴾

27. Na mchanganyo wake ni (maji ya) Tasnymu

وَمِزَاجُهُ مِن تَسْنِيمٍ ﴿٢٧﴾

28. (Hiyo Tasnimu ni) chemchem watakayoinywa (watu) waliokurubishwa (na Mwenyezi Mungu).

عَيْنًا يَشْرَبُ بِهَا الْمُقَرَّبُونَ ﴿٢٨﴾

---

14. Mtu akifanya jambo baya mara ya kwanza (wala asitubie), huingia kidoa cheusi katika moyo wake; na kila akizidi maovu, na kile kidoa huzidi kupanuka, na huendelea hata kikafinika moyo wote. Na hiyo ndio "RAN" Na moyo ukifikilia hadi hiyo huwa haujali tena kufanya maovu, na hata ukinyoshwa haunyoki!

26. Hapa pana mahimizo ya watu kushindana katika kufanya mema ili wapate hizo neema walizoandaliwa watu wema. Na muradi ni kila mtu kujipinda katika kufanya Ibada na kheri nyenginezo. La si kufanya vinara vya Maulidi na Dhikiri wakashindana kwa midundo na mingurumo; bali hayo yakiwa yatasababisha utesi baina ya Waislamu yatakuwa ni haramu kamwe.

28. Wenye kukurubishwa hapa ni watu wema walio na daraja kubwa mbele za Mwenyezi Mungu.

إن الذين أجرموا كانوا من الذين آمنوا يضحكون ﴿٢٩﴾

29. Kwa hakika wale waliokuwa wanafanya madhambi walikuwa wakiwacheka walioamini

وإذا مروا بهم يتغامزون ﴿٣٠﴾

30. Na wanapopita karibu yao, wanakonyezana (kwa kuwachokoza).

وإذا انقلبوا إلى أهلهم انقلبوا فكهين ﴿٣١﴾

31. Na wanaporudi kwa watu wao hurudi na hali ya kuwa wamefurahi (kwa kuwaudhi)

وإذا رأوهم قالوا إن هؤلاء لضالون ﴿٣٢﴾

32. Na wanapowaona husema: "Hakika hawa ndio (khasa) waliopotea." (Ati Waislamu wamepotea!)

وما أرسلوا عليهم حافظين ﴿٣٣﴾

33. Na wao makafiri hawakupelekwa kuwa walinzi juu yao (Waislamu).

فاليوم الذين آمنوا من الكفار يضحكون ﴿٣٤﴾

34. Basi leo walioamini watawacheka waliokufuru

على الأرائك ينظرون ﴿٣٥﴾

35. (Watakuwa) Juu ya viti vya fakhari, wakitazama (neema zao).

هل ثوب الكفار ما كانوا يفعلون ﴿٣٦﴾

36. Je, makafiri wamepewa malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda? (Ndiyo wamelipwa kwa yale waliyokuwa wakiyatenda).

---

31. Huona raha kwa kule kuwacheka Islamu na kuwacheza shere.

33. Maana yake: Hao makafiri wasemao maneno hayo Mungu hakuwapeleka kuwatunza wenye kuamini. Basi inawahusu nini wakipotea au wakiongoka?

34-36. Maana yake: Wenye kuamini, Siku ya Kiama watakuwa juu ya makochi yao wakiwacheka makafiri — kama vile walivyokuwa wakiwacheka wao Duniani—na kuwatazama kama wamekwishalipwa kwa waliyokuwa wakiyatendea.

اٰيَاتُهَا ٢٥ (٨٤) سُوْرَةُ الْاِنْشِقَاقِ مَكِّيَّةٌ (٨٣) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 25* *Ina Kara 1*

# SURATUL INSHIQAQ

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye Kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

اِذَا السَّمَآءُ انْشَقَّتْ (١)

1. Mbingu zitakapopasuka

وَاَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ (٢)

2. Na zitakapokinga shikio kwa Mola wake (kusikiliza amri); na zimepasiwa (na kusikiliza)

وَاِذَا الْاَرْضُ مُدَّتْ (٣)

3. Na ardhi itakapotandazwa (itakaponyoshwa).

وَاَلْقَتْ مَا فِيْهَا وَتَخَلَّتْ (٤)

4. Na kuvitoa vilivyokuwa ndani yake, ikawa tupu

وَاَذِنَتْ لِرَبِّهَا وَحُقَّتْ (٥)

5. Na ikakinga shikio kwa Mola wake; na imepasiwa (na kusikiza). (Wakati huo kila mmoja atalipwa kwa lake).

يٰۤاَيُّهَا الْاِنْسَانُ اِنَّكَ كَادِحٌ اِلٰى رَبِّكَ كَدْحًا فَمُلٰقِيْهِ (٦)

6. Ewe mtu! Hakika wewe unajikusurukusuru (katika kufanya mambo yako) mpaka (siku utakapokutana na) Mola wako; basi (amali zako hizo) utazikuta.

فَاَمَّا مَنْ اُوْتِيَ كِتٰبَهٗ بِيَمِيْنِهٖ (٧)

7. Ama atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kulia

فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَّسِيْرًا (٨)

8. Basi yeye atahisabiwa hisabu nyepesi.

وَّيَنْقَلِبُ اِلٰۤى اَهْلِهٖ مَسْرُوْرًا (٩)

9. Na atarudi kwa watu wake (Peponi), na hali ya kuwa ni mwenye furaha.

وَاَمَّا مَنْ اُوْتِيَ كِتٰبَهٗ وَرَآءَ ظَهْرِهٖ (١٠)

10. Lakini atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake

---

4. Katika jumla ya vituko vya Siku ya Kiama ni kutetemeka Ardhi kwa nguvu sana hata iwachane na majabali, ambayo ndiyo vigingi vyake vya kuzuilia isitoke katika Falaki yake, na kwa sababu hiyo itavutika inyoke, na vilivyomo ndani vyote vitatokea nje, Ardhi iwe tupu.

5. Baada ya Mwenyezi Mungu kusema hivi, hakusema itakuwa nini. Amemuachia mwenyewe mwanadamu afikiri litakalokuwa vitakapotuka vituko hivyo, ili azidi kufanya khofu.

6. Maana yake: Ewe mwanaadamu! Wewe wajitahidi kufanya mema na maovu, na huku unakwenda kwa Mola wako (yaani umri wako unamalizika kidogo kidogo, na ukisha nawe utakufa wende kwa Mola wako). Hapo utakwendakuta amali zako zote ulizojipinda kuzifanya—ikiwa ni za kheri au ni za shari.

7. Siku ya Hisabu kila mtu atapewa daftari lake kama ilivyotaja Aya ya 10 ya *Suratut Takwyr*, basi kuna watakaopewa kwa upande wa kulia; na hao ndio watu wema; kuna watakaopewa kwa upande wa kushoto na kwa migongo; na hao ndio watu waovu.

8. Watu, kuna watakaohisabiwa pasi na kuhojiwa, kwa kila walilolitenda, bali watatajiwa mema yao na maovu yao, kisha watasamehewa yale maovu walipwe kwa mema. Hao ndio watu wema, na hiyo ndiyo "Hisabu Nyepesi." Kuna na wengine watahisabiwa pamoja na kuhojiwa kwa kila walilolitenda moja moja. Hao ndio watu waovu, na hiyo ndiyo. "Hisabu Nzito."

11. Basi yeye atayaita mauti (yamjie; ili afe apumzike, wala hayatamjia)

فَسَوْفَ يَدْعُوا ثُبُورًا ﴿١١﴾

12. Na ataingia Motoni.

وَيَصْلَىٰ سَعِيرًا ﴿١٢﴾

13. Maana alikuwa na furaha (za maasia) pamoja na watu wake

إِنَّهُ كَانَ فِي أَهْلِهِ مَسْرُورًا ﴿١٣﴾

14. (Na) alidhani kuwa hatarejea (kwa Mwenyezi Mungu).

إِنَّهُ ظَنَّ أَن لَّن يَحُورَ ﴿١٤﴾

15. Kwa nini (asirejee)? Mola wake alikuwa akimuona; (kwa hivyo atamlipa kwa kila aliyoyafanya).

بَلَىٰ إِنَّ رَبَّهُ كَانَ بِهِ بَصِيرًا ﴿١٥﴾

16. Basi Ninaapa kwa wekundu (wa jua lichwapo)

فَلَا أُقْسِمُ بِالشَّفَقِ ﴿١٦﴾

17. Na kwa usiku na unavyovikusanya

وَاللَّيْلِ وَمَا وَسَقَ ﴿١٧﴾

18. Na kwa mwezi unapokamilika

وَالْقَمَرِ إِذَا اتَّسَقَ ﴿١٨﴾

19. Mutakutana na hali baada ya hali.

لَتَرْكَبُنَّ طَبَقًا عَن طَبَقٍ ﴿١٩﴾

20. Basi wana nini hawaamini?

فَمَا لَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٠﴾

21. Na wanaposomewa Qurani hawanyenyekei?

وَإِذَا قُرِئَ عَلَيْهِمُ الْقُرْآنُ لَا يَسْجُدُونَ ﴿٢١﴾

22. Lakini wale waliokufuru wanakadhibisha (tu).

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا يُكَذِّبُونَ ﴿٢٢﴾

23. Na Mwenyezi Mungu Anajua wanayoyakusanya.

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يُوعُونَ ﴿٢٣﴾

24. Basi wabashirie adhabu iumizayo

فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٤﴾

25. Isipokuwa wale walioamini na kutenda vitendo vizuri; hao watakuwa na ujira usiokoma (usiomalizika).

إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٢٥﴾

---

17. Ada ya wanaadamu na hayawani wengine ni kutapanyika mchana kwa sababu ya kutafuta maisha na ukiingia usiku wanakusanyika, ndio mapendeleo ya "usiku na unavyovikusanya."

19. Yaani: baada ya uhai mtapambana na mauti, kisha mpambane na uhai mwengine, kisha mpambane na Hisabu, na mengine katika mambo mazito ya Siku ya Kiama.

23. Yaani: "wanayoyakusanya" katika nyoyo zao kama kufuru na hasadi na kumchukia Mtume (s.a.w.) na mengineyo.

25. Aya hii yaonesha kwamba kuamini kutupu hakutoshi kumuepusha mtu na adhabu ya Akhera, bali yamlazimu kufanya na amali njema; na katika Qurani yote kila walipotajwa "Wenye kuamini" wamefungamanishwa na "kutenda vitendo vizuri."

آيَاتُهَا ٢٢ (٨٥) سُورَةُ الْبُرُوجِ مَكِّيَّةٌ (٢٧) رُكُوعُهَا ١

*Ina Aya 22* *Ina Kuru 1*

## SURATUL BURUJ

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa mbingu zenye Buruji (nyota)

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْبُرُوجِ ۝١

2. Na kwa siku iliyoahidiwa (kuwa itafika, nayo ni Siku ya Kiama)

وَالْيَوْمِ الْمَوْعُودِ ۝٢

3. Na Mwenye kushuhudia na kishuhudiwacho.

وَشَاهِدٍ وَمَشْهُودٍ ۝٣

4. (Kuwa) wameangamizwa watu waliowaadhibu Waislamu katika mahandaki.

قُتِلَ أَصْحَابُ الْأُخْدُودِ ۝٤

5. Yenye Moto wenye kuni (nyingi)

النَّارِ ذَاتِ الْوَقُودِ ۝٥

6. Walipokuwa wamekaa hapo

إِذْ هُمْ عَلَيْهَا قُعُودٌ ۝٦

7. (Waliangamizwa makafiri hao pale wakati walipokuwa) wanatazama yale wanayowafanyia hao Waislamu (walipokuwa wakiwaadhibu).

وَهُمْ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ بِالْمُؤْمِنِينَ شُهُودٌ ۝٧

---

1. *Buruji* ni nyota ambazo zimekaa vikundi vikundi, kila kikundi huitwa *Burji*, na *Buruji* zote ni 12: Sita ziko Kaskazini ya Ikweta (Equator), na sita ziko Kusini yake.

3. Katika "Mwenye kushuhudia na kishuhudiliwacho" anaingia kila atakaye kuwa shahidi na kushudiliwa Siku ya Kiama; kama Mitume, watashuhudilia umati wao kwa wema wao na uwovu wao; mwahali mwa Ibada; mtawashuhudilia kwa wema wenye kuabudu; mwahali mwa maasia; mtawashuhudilia kwa uovu wenye kuasi; na hata viungo vya mtu na ngozi ya mwili wake pia Siku hiyo vitatoa ushahidi juu ya mtu huyo. Basi yataka mtu akiazimia kufanya maasi akumbuke kuwa ana mashahidi kadha wa kadha wamuonao, na Siku ya Kiama watasimama mbele za Mwenyezi Mungu watowe ushahidi wao juu ya mtu yule!

4. Wakati Mayahudi wa Najrani walipoingia katika Umasihia (kabla ya kuja Uislamu na kabla ya Umasihia kuharibiwa), alipata habari mfalme wao, Dhu-Nuwas; akaja Najrani na jeshi kubwa, akawalazimisha watu wa Najrani warudi katika Uyahudi; nao wasikubali. Dhu-Nuwas akachimba handaki kubwa akatia kuni, akawasha moto. Akawa humshika mmoja mmoja katika wale Wamasihia wa Najrani akiwatupa katika handaki lile, na yeye na watu wake wamekaa pambizoni mwa handaki watafaraji.

Katika Sura hii Mwenyezi Mungu Ametaja kisa hiki, pamoja na kuashiria kisa cha Firauni na Thamudi (kama utakavyoona katika Aya zijazo) ili kumliwaza Mtume na Sahaba zake wajue kwamba tabu iwapatayo kwa makafiri, imeanza kuwafikilia ndugu zao waliotangulia.

Katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya ni ya 5 wamesema uwongo kabisa. Wafasiri wote na wanavyuoni wa Tarehe wote wamehadithia kuwa mambo haya yalitokea kabla ya Nabii Muhammad (s.a.w.). Hakuna mmoja aliyesema kuwa haya yatatokea baadaye; hata leo ndiyo wao wanasema kuwa haya yamemhusu mtu wao ili wamdaiae Utume. Na mara ya mwisho tulipojibu kwa urefu ukafiri wa kudai Utume baada ya Nabii Muhammad (s.a.w.) ni katika marejezo ya Aya ya 40 ya *Suratul Ahzaab*.

8. Nao hawajaona baya lolote kwao (Waislamu) ila kumuamini Mwenyezi Mungu Mwenye kushinda (na) Mwenye kusifiwa

وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَن يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٨﴾

9. Ambaye ni Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuona kila kitu.

الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٩﴾

10. Hakika wale waliowaadhibu Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, kisha wasitubie basi watapata adhabu ya Jahanamu na watapata adhabu ya kuungua (barabara).

إِنَّ الَّذِينَ فَتَنُوا الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ لَمْ يَتُوبُوا فَلَهُمْ عَذَابُ جَهَنَّمَ وَلَهُمْ عَذَابُ الْحَرِيقِ ﴿١٠﴾

11. Hakika wale walioamini na kutenda vitendo vizuri bila shaka watapata Mabustani yenye mito ipitayo mbele yake. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْكَبِيرُ ﴿١١﴾

12. Hakika kutesa kwa Mola wako ni kukali (sana).

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿١٢﴾

13. Yeye ndiye aliyeanzisha (viumbe) na Ndiye atakayewarejeza.

إِنَّهُ هُوَ يُبْدِئُ وَيُعِيدُ ﴿١٣﴾

14. Naye ni Mwingi wa msamaha Mpenda (waja Wake)

وَهُوَ الْغَفُورُ الْوَدُودُ ﴿١٤﴾

15. Mwenye kiti cha enzi kitukufu

ذُو الْعَرْشِ الْمَجِيدُ ﴿١٥﴾

16. Mwingi wa kutenda Alipendalo.

فَعَّالٌ لِّمَا يُرِيدُ ﴿١٦﴾

---

8. Maana yake: Hapana lililomchukiza Dhu-Nuwas na wafuwasi wake kwa watu wa Najrani hata wakawakutisha adhabu hiyo ila ni kuwa wao wamemuamini Mwenyezi Mungu tu, Hapana jengine!

10. Makusudio ya kuadhibu hapa ni kuwaudhi wenye kuamini na kuwatenza nguvu ili wawache dini yao warudi katika ukafiri. Na maneno haya kama ambavyo yanawahusu wale wenye handaki waliotangulia kutajwa, kadhalika yanawahusu na makafiri wa Makka waliokuwa wakiwaadhibu Islamu kwa namna namna za udhia ili wawalazimishe kurejea katika ukafiri. Na kama ambavyo yanahusu hao, kadhalika yanawakhusu kila watakaofanya kama hayo.

12-16. Mwenyezi Mungu baada ya kuwaliwaza Islamu kwa kuwatajia mambo yaliyowafika ndugu zao waliotangulia, sasa anawaliwaza tena kwa Aya hizi, pamoja na kuwasubirisha, kwa kuwaonesha Nguvu Zake Kubwa na Ufalme Wake Mtukufu. Wajue kwamba hao makafiri wajionao wana nguvu za kuwaadhibu wenziwao, Yeye hawamshindi. Atakapopenda Atawapatiliza kwa adhabu ya Dunia na Akhera, au mojawapo. Na kwa kuwa Yeye ni "Mwingi wa Maghufira" na "Mwenye Mapenzi," Atakapopenda Atawageuza nyoyo hao makafiri, walikubali hilo walikataalo leo, na kuliletea hilo walipigalo vita. Na kwa Uweza Wake Mkubwa,Ameyafanya yote mawili. Baada ya myaka michache Aliwapa nguvu hao waliokuwa wanyonge. Akawapatiliza baadhi ya makafiri kwa adhabu ya Dunia na Akhera, kama Abu Jahl na wenziwe waliokuwa wakimuudhi sana Mtume na Sahaba zake. Na baadhi yao Akawageuza nyoyo zao wakaingia katika Dini ya Uislamu, wakasimama kuitetea kwa roho zao na mali yao pia; hata wakafa vitani na huku wanatamani warudi wapiganie Dini!

13. Maana ya Aya hii, ni kuwa Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye kuanza kuumba kila kitu, na Ndiye Atakayevirejeza katika uhai baada ya kufa.

17. Je, zimekuwasilia habari za majeshi ya makafiri

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ الْجُنُودِ ﴿١٧﴾

18. Firauni na Thamudi?

فِرْعَوْنَ وَثَمُودَ ﴿١٨﴾

19. Lakini waliokufuru wamo katika kukadhibisha tu

بَلِ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي تَكْذِيبٍ ﴿١٩﴾

20. Na Mwenyezi Mungu Amewazunguka kote kote (hawawezi kuikimbia adhabu Yake).

وَاللَّهُ مِن وَرَائِهِم مُّحِيطٌ ﴿٢٠﴾

21. Bali hii ni Qurani tukufu

بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ ﴿٢١﴾

22. (Iliyotolewa) katika huo ubao uliohifadhiwa, (wa Mwenyezi Mungu).

فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ ﴿٢٢﴾ ع

---

17,18. Maana ya Aya mbili hizi ni haya: Mwenyezi Mungu Anamwambia Mtume Wake: Jee, imekufikilia khabari ya Askari wa Firauni na Thamudi namna walivyokadhibisha Mitume yao, na kuwaudhi walioamini katika wao na namna Mwenyezi Mungu Alivyowapatiliza kwa madhambi yao, Akamtotesha Firauni na askari zake katika bahari na akawaangamiza Thamudi. Na Thamudi ni kabila ya uma wa Nabii Salih.

20. Na muradi wake hapa ni kuwa hao makafiri wamo katika kabdhi ya Mwenyezi Mungu na tasarufi Yake; hawana pa kukimbilia.

22. Maana yake: Hii wanayosomewa makafiri ni Qurani tukufu, iliyo katika Ubao uliyohifadhiwa huko mbinguni, si maneno ya watu wa kale kama wadhanivyo wao. Na huo "Ubao wenye kuhifadhiwa" anayejua namna yake ni Yeye Mwenyewe tu Mwenyezi Mungu. Na ambalo linatupasa sisi ni kuamini tu kuwa uko siyo kuijua KAYFIA yake.

Katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya ya 23 wamegeuza muradi wa neno "*Lawhin Mahfuudh.*"

اٰيَاتُهَا ١٧ (٨٦) سُوْرَةُ الطَّارِقِ مَكِّيَّةٌ (٣٦) رُكُوْعُهَا ١

Ina Aya 17 — Ina Kara 1

## SURATUT TARIQ

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Naapa kwa mbingu na kwa kijacho usiku

وَالسَّمَآءِ وَالطَّارِقِ ۝١

2. Na nini kitakachokujulisha kipi hicho kujacho usiku (nilichokikusudia)!

وَمَآ اَدْرٰىكَ مَا الطَّارِقُ ۝٢

3. Ni nyota inayong'ara sana!

النَّجْمُ الثَّاقِبُ ۝٣

4. (Naapa ya kuwa) hakuna nafsi yoyote ila inayo mchungaji juu yake, (anayetazama amali zake).

اِنْ كُلُّ نَفْسٍ لَّمَّا عَلَيْهَا حَافِظٌ ۝٤

5. Hebu naajitazame mtu, ameumbwa kwa kitu gani

فَلْيَنْظُرِ الْاِنْسَانُ مِمَّ خُلِقَ ۝٥

6. Ameumbwa kwa maji yatokayo kwa kuchupa.

خُلِقَ مِنْ مَّآءٍ دَافِقٍ ۝٦

7. Yatokayo katikati ya mifupa ya mgongo na kifua (Mbavu).

يَّخْرُجُ مِنْۢ بَيْنِ الصُّلْبِ وَالتَّرَآئِبِ ۝٧

8. Kwa yakini Yeye Ana uweza wa kumrudisha.

اِنَّهٗ عَلٰى رَجْعِهٖ لَقَادِرٌ ۝٨

9. Siku zitakapodhihirishwa siri

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَآئِرُ ۝٩

10. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi.

فَمَا لَهٗ مِنْ قُوَّةٍ وَّلَا نَاصِرٍ ۝١٠

11. Naapa kwa mawingu yanayoleta mvua

وَالسَّمَآءِ ذَاتِ الرَّجْعِ ۝١١

12. Na kwa ardhi inayopasuka (ikatoa mimea)

وَالْاَرْضِ ذَاتِ الصَّدْعِ ۝١٢

13. Kuwa hii (Qurani) ni kauli ipambanuayo haki

اِنَّهٗ لَقَوْلٌ فَصْلٌ ۝١٣

14. Wala si mzaha.

وَّمَا هُوَ بِالْهَزْلِ ۝١٤

15. Hakika wao wanafanya hila

اِنَّهُمْ يَكِيْدُوْنَ كَيْدًا ۝١٥

---

4. Mwenye kuichunga nafsi ni mwenye kuhifadhi amali zake za kheri na za shari. Na hii ni kazi ya wale malaika wawili: "Rakib" na "Atid."

8. Maana yake hapana shaka kwamba Mwenye kuweza kumuumba mwanaadamu kwa tone la manii, ni muweza zaidi wa kumrejeza atakapokufa.

10. Yaani Siku hiyo mtu hatakuwa na wa kumnusuru.

12. Makusudio ni pasuko ambazo husababishwa na mimea wakati ikichipua.

16. Na Mimi nazipindulia mbali hila zao.

وَأَكِيدُ كَيْدًا ﴿١٦﴾

17. Basi wape makafiri muda — wape muda kidogo (wataona sasa hivi).

فَمَهِّلِ الْكَافِرِينَ أَمْهِلْهُمْ رُوَيْدًا ﴿١٧﴾ ع

---

15-16. Maana hao makafiri wanafanya vitimbi ili wazime Nuru ya Qurani na kujaribu kuwarejeza wenye kuamini katika ukafiri na kutaka kumuangamiza Mtume s.a.w.; na Mwenyezi Mungu anawafanyia vitimbi kwa kuwarusha patupu na kuwavunjia wayafanyayo, na kuwarejezea wenyewe vitimbi vyao viwe ni sababu ya kuzidishiwa adhabu.

*Ina Aya 19*

## SURATUL A'LAA

*(Imeteremka Makka)*

*Ina Kura 1*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Litukuze jina la Mola wako aliye Mtukufu

سَبِّحِ اسْمَ رَبِّكَ الْاَعْلَى ۝١

2. Aliyeumba (kila kitu na) akakitengeneza

الَّذِيْ خَلَقَ فَسَوّٰى ۝٢

3. Na akakikadiria (kila kimoja jambo lake) na akakiongoza (kufanya jambo hilo)

وَالَّذِيْ قَدَّرَ فَهَدٰى ۝٣

4. Na aliyeotesha Ndisha (Malisho)

وَالَّذِيْٓ اَخْرَجَ الْمَرْعٰى ۝٤

5. Kisha akaifanya mikavu yenye kupiga weusi.

فَجَعَلَهٗ غُثَاۗءً اَحْوٰى ۝٥

6. Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau.

سَنُقْرِئُكَ فَلَا تَنْسٰٓى ۝٦

7. Ila Akipenda Mwenyezi Mungu; Yeye Anajua yaliyo dhahiri na yaliyofichikana.

اِلَّا مَا شَاۗءَ اللّٰهُ ۭ اِنَّهٗ يَعْلَمُ الْجَهْرَ وَمَا يَخْفٰى ۝٧

8. Nasi Tutakusahilishia (kuitangaza) dini iliyo nyepesi (dini ya Uislamu).

وَنُيَسِّرُكَ لِلْيُسْرٰى ۝٨

9. Basi waidhishe ikiwa utafaa waadhi

فَذَكِّرْ اِنْ نَّفَعَتِ الذِّكْرٰى ۝٩

---

1. Maana ya kumtukuza Mwenyezi Mungu, ni kuitakidi kwamba Yeye Ametakata na kila sifa mbaya na isiyokuwa laiki Yake, kama kushabihiana na viumbe, na kuzaa au kuzaliwa, na kuwa na mke, na kuwa na mshirika katika uungu. . .

3. Mwenyezi Mungu baada ya kuumba viumbe hakuwatupilia mbali akawawacha hawajui la kufanya, bali kila kiumbe amemkadiria lililo na maslaha yake kisha Akamuongoza katika jambo hilo; akalijuwa, akalifuwata. Akamuonesha na lililo na madhara naye ili ajiepushe nalo.

6. Mtume (s.a.w.) alikuwa mwanaadamu, kama wanaadamu wengine, na alikuwa amesifika na kila sifa ya wanaadamu, kama kupenda na kuchukia, na kusahau, na kukumbuka. . . Na imetokea mara moja kusahau, na kusali rakaa tatu katika sala ya rakaa nne. Kwa sababu hii alikuwa, wakati akiteremshiwa Qurani na Jibrili akijipinda sana na kukariri kile alichosomewa mara kwa mara, kuchelea asije akasahau. Basi hapa Mwenyezi Mungu Anamkataza Mtume Wake asijipe taklifu hiyo, pamoja na kumpa waadi kuwa hatasahau. Na Akatimiza waadi Wake, akawa Mtume (s.a.w.) huteremshiwa Sura ndefu ndefu, naye akiwasomea Masahaba kama alivyosomewa pasi na kuzidisha au kupunguza kitu, pamoja na kuwa yeye hajui kusoma wala kuandika.

7. Mwenyezi Mungu kusema hivi si maana yake kuwa Atapenda kumsahaulisha Mtume Wake kitu katika Qurani, bali ni dalili kuwa hatasahau kabisa. Na Waarabu hutumia maneno ya namna hii katika kukanusha jambo (Taz. Baidhawi).

8. Makusudio ya "Nyepesi" ni Sharia ya Kiislamu ambayo haina taklifu zilizokuwako katika Sharia zilizotangulia, na ambayo ndiyo ya kuwafaa watu wote, zamani zozote na mahali popote.

9. Si makusudio kuwa Mtume asitoe waadhi mpaka ajue kuwa waadhi wake utafaa, bali makusudio ni kuamrishwa atoe waadhi tu, ukifaa au usifae kama zifahamishavyo Aya zijazo. Mseino wa namna hii Waarabu huita "iktifa" (Tazama Sawi).

| | |
|---|---|
| 10. Bila shaka atakumbuka mwenye kumuogopa (Mwenyezi Mungu) | سَيَذَّكَّرُ مَن يَخْشَىٰ ﴿١٠﴾ |
| 11. Na mwingi wa mateso atajitenga mbali nayo hayo (mawaidha) | وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَى ﴿١١﴾ |
| 12. Ambaye atauingia Moto mkubwa. | الَّذِي يَصْلَى النَّارَ الْكُبْرَىٰ ﴿١٢﴾ |
| 13. Kisha humo hatakufa wala hatakuwa hai. | ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿١٣﴾ |
| 14. Hakika amekwishafaulu aliyejitakasa (na mabaya) | قَدْ أَفْلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ﴿١٤﴾ |
| 15. Akakumbuka jina la Mola wake na akasali. | وَذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّىٰ ﴿١٥﴾ |
| 16. Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia. | بَلْ تُؤْثِرُونَ الْحَيَوٰةَ الدُّنْيَا ﴿١٦﴾ |
| 17. Hali ya kuwa ya Akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu. | وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿١٧﴾ |
| 18. Hakika haya (mnayoambiwa humu katika Qurani) yamo katika Vitabu vilivyotangulia | إِنَّ هَٰذَا لَفِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٨﴾ |
| 19. Vitabu vya Ibrahimu na Musa (na wengineo). | صُحُفِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾ |

---

11. "Mateso" ni "Tabu na mashaka." Na Mwenyezi Mungu Amemwita kafiri "mwingi wa mateso" kwa kuwa ana mateso makubwa duniani na Akhera pia. Mateso ya Akhera ni kama tuyajuayo ya adhabu alizoandaliwa. Ama mateso ya Ulimwenguni ni kuwa hana jambo la kumliwaza wakati akipatikana na msiba au tabu yoyote. Islamu akifiliwa, mathalan, hujiliwaza kwa Imani yake kwamba umri wa mtu hauzidi wala haupungui, na watu wote watakufa watakapomaliza umri wao. Lakini kafiri hafikiri hayo, bali huuma vidole na kuwatukana madakitari kuwa hawajui kitu, na lau kama wangefanya kadha, mtu wake asingekufa. Islamu akipatikana na ufakiri hujiliwaza kwa subira na kuamini kuwa mambo yote yapo katika tasarufi ya Mwenyezi Mungu; pamoja na kutaraji kuwa leo au kesho Mwenyezi Mungu Atamtermshia Rehema Yake. Lakini asiyekuwa na Imani huona amedhulumiwa, akajaribu kutafuta mali kwa njia zisizofaa, na akikosa akamlaumu huyu na kumpiga vita yule; na akajiona dhalili mbele za kila tajiri, hata lau kama anamwambia "nisujudie" angemsujudia! Na kila siku huwa akikonda kwa hasadi; na pengine akajiua, kama tunavyoona kila siku. Na hakuna mateso makubwa kama mateso ya moyo. Ukitazama Aya mbili hizi 10 na 11, utaona zinatia nguvu tuliyotangulia kuyasema kwamba Mtume ameamriwa kutoa waadhi, ukimfaa mwenye kuwaidhiwa au usimfae; kisha mwenye kumcha Mungu atawaidhika, na mwingi wa mateso atajiepusha nao.

13. Yaani hatakufa akapumzika wala hatakuwa hai akanufaika kwa uhai wake huo.

14. Yaani mwenye kujitakasa kwa kuwacha ukafiri na kwa kuwacha kumuasi Mola wake; na maasi ya peke yake yatosha kuzuilia waadhi usiingie katika moyo wa mtu. (Tazama Maelezo 14, Sura ya *Mutaffifyn).*

18. Maana yake: Haya mliyoambiwa kwamba mwenye kufuzu ni mwenye kujitakasa, akamkumbuka Mola wake, akasali; na kwamba Akhera ni bora kuliko Ulimwengu; yote haya yametangulia kutajwa katika vitabu vilivyotangulia, si kuwa yameanza kutajwa katika Qurani.

اياتها ٢٦ (٨٨) سورة الغاشية مكية (٦٨) ركوعها ١

*Ina Aya 26*

## SURATUL GHASHIYAH

*(Imeteremka Makka)*

*Ina Kara 1*

Kwajina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Je! Imekuwasilia habari ya msiba utakaowafudikiza (viumbe)?

هل أتاك حديث الغاشية ١

2. Nyuso siku hiyo ni zenye kudhalilika

وجوه يومئذ خاشعة ٢

3. Ni zenye kufanya kazi ngumu kabisa (huko Motoni), zichoke (kuchoka kusikokuwa na mfano)

عاملة ناصبة ٣

4. Waingie katika moto uwakao kweli kweli

تصلى نارا حامية ٤

5. Watanyweshwa (humo) katika chemchem zichemkazo barabara.

تسقى من عين آنية ٥

6. Hawatakuwa na chakula isipokuwa cha miba

ليس لهم طعام إلا من ضريع ٦

7. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa.

لا يسمن ولا يغني من جوع ٧

8. Nyuso (nyingine) siku hiyo ni zenye kumemetuka

وجوه يومئذ ناعمة ٨

9. Zitakuwa radhi kwa ajili za amali zao

لسعيها راضية ٩

10 Zitakuwemo katika Pepo iliyotukufu

في جنة عالية ١٠

11. Hazitasikia humo yasiyo na maana.

لا تسمع فيها لاغية ١١

12. Humo muna chemchem zinazotiririka (kwa vizuri).

فيها عين جارية ١٢

13. Humo muna viti vya fahari vilivyoinuka juu

فيها سرر مرفوعة ١٣

---

2. Muradi wa "Nyuso" hapa, (wujuuh) ni "wenye nyuso." Na waliokusudiwa hapa ni watu waovu. Na Mwenyezi Mungu Ametaja nyuso kwa kuwa ndipo mahali patukufu katika umbo la mwanadamu, na ndipo palipo na sura zake.

7. Waarabu hutumia maneno kama haya wakitaka kuonesha kuwa kitu hakina manufaa hata kidogo.

8. Na hapa mapendeleo ya nyuso ni yale yale, na waliokusudiwa ni watu wema.

9. Maana ya kuwa radhi hapa ni kupendezewa. Yaani watu wema watapendezewa na amali zao walizozifanya ulimwenguni watakapokuta majaza mema watakayojaziwa Akhera.

12-16. Hakika ya starehe za Akhera ni kama alivyotwambia Mtume (s.a.w.) kwamba Peponi kuna vitu ambavyo jicho halijaona, wala shikio halijasikia, wala havijapita katika fikra ya mtu. Basi starehe hizi alizozitaja Mwenyezi Mungu hapa, ni kadri ya kupigia mifano tu katika vitu tuvijuavyo.

| | |
|---|---|
| 14. Na gilasi zilizowekwa (vizuri) | وَأَكْوَابٌ مَّوْضُوعَةٌ ﴿١٤﴾ |
| 15. Na matakia yaliyopangwa safu safu | وَنَمَارِقُ مَصْفُوفَةٌ ﴿١٥﴾ |
| 16. Na mazulia yaliyotandikwa (vizuri). | وَزَرَابِيُّ مَبْثُوثَةٌ ﴿١٦﴾ |
| 17. Je! Hawawatazami ngamia jinsi walivyoumbwa? | أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى الْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿١٧﴾ |
| 18. Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa? | وَإِلَى السَّمَاءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ﴿١٨﴾ |
| 19. Na milima jinsi ilivyothubutishwa? | وَإِلَى الْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿١٩﴾ |
| 20. Na ardhi jinsi ilivyotandazwa? (Basi aliyeyafanya hayo kutamshinda kufufua Binadamu) | وَإِلَى الْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Basi kumbusha; hakika wewe ni Mkumbushaji (tu). | فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنتَ مُذَكِّرٌ ﴿٢١﴾ |
| 22. Wewe si mwenye kuwatenza nguvu | لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٢﴾ |
| 23. Lakini anayerudi nyuma na kukufuru | إِلَّا مَن تَوَلَّىٰ وَكَفَرَ ﴿٢٣﴾ |
| 24. Mwenyezi Mungu atamuadhibu adhabu iliyo kubwa. | فَيُعَذِّبُهُ اللَّهُ الْعَذَابَ الْأَكْبَرَ ﴿٢٤﴾ |
| 25. Hakika marejeo yao ni Kwetu | إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٢٥﴾ |
| 26. Kisha, bila shaka, hisabu yao ni juu Yetu. | ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم ﴿٢٦﴾ |

---

17-20. Mwenyezi Mungu anawambia makafiri watazame umbo la ngamia, na mbingu, na majabali na ardhi, kisha wafikiri na wazingatie, waone kuwa aliyeumba vitu hivyo ni muweza kabisa — wa kuwarejeza wanaadamu. Na sababu ya Mwenyezi Mungu kutaja vitu hivi, ni kuwa maneno haya ingawa yamhusu kila mtu — lakini walikuwa wakiambiwa makafiri wa Makka, ambao vitu hivi ndivyo vilivyokuwa katika macho yao kila wakati.

22. Aya hii yatosha kuwarudi maadui wa Dini wasemao kwamba "Dini ya Uislamu imesimama kwa upanga" kwa maana ya kuwa "imetumia nguvu katika kuwatia watu katika dini." Si ajabu maadui wa dini kuitia ila Dini ya Kiislamu, lakini ajabu ni kutoka uzushi huu katika vinywa vya wanaodai kuwa ni "Islamu"! Kweli wako baadhi ya wanavyuoni waliosema kuwa dini imesimama kwa upanga, lakini si kwa maana hayo waliyochukulia hao maadui wasiojua kitu katika dini ya Islamu ila wafuata madanganyo ya wakubwa wao tu. Makusudio ya wanavyuoni waliosema hivyo ni kuwa "Imejitetea kwa upanga." Na kujitetea siko kutumia nguvu katika kusilimisha watu, wala Uislamu wa nguvu haukubaliwi kamwe. Na kila ajuae tarekhe ya Uislamu, japo kidogo tu, anajua kwamba Waislamu hawakuamrishwa jihadi ila walipoanza kutaadiwa na makafiri. Na viko visa mashuhuri vya masahaba wa Madina waliyotaka kuwatia watoto wao kwa nguvu katika Dini ya Uislamu, wakazuiliwa. Basi mtu asemae maneno haya ima ni mjinga sana wa Dini ya Kiislamu, au ni mwendawazimu.

ايَاتُهَا ٣٠ (٨٩) سُوْرَةُ الْفَجْرِ مَكِّيَّةٌ (١٠) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 30* **SURATUL FAJR** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

| | |
|---|---|
| Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo. | بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ |
| 1. Naapa kwa alfajiri | وَالْفَجْرِ ۝١ |
| 2. Na kwa masiku kumi | وَلَيَالٍ عَشْرٍ ۝٢ |
| 3. Na kwa "shafi" na witri | وَّالشَّفْعِ وَالْوَتْرِ ۝٣ |
| 4. Na kwa usiku unapopita. | وَالَّيْلِ إِذَا يَسْرِ ۝٤ |
| 5. (Naapa nasema kuwa) kuna katika haya (kuonekana) kiapo kwa mwenye akili (akaogopa). | هَلْ فِىْ ذٰلِكَ قَسَمٌ لِّذِىْ حِجْرٍ ۝٥ |
| 6. Je! Hukuona jinsi Mola wako Alivyowafanya Adi (Iram) | أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ۝٦ |
| 7. (Adi) Iram (waliokuwa) wana majumba marefu marefu | إِرَمَ ذَاتِ الْعِمَادِ ۝٧ |
| 8. Ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji (mingine) | الَّتِىْ لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِى الْبِلَادِ ۝٨ |
| 9. Na Thamudi waliochonga majabali (wakayafanya majumba) katika uwanja (wao) | وَثَمُوْدَ الَّذِيْنَ جَابُوا الصَّخْرَ بِالْوَادِ ۝٩ |
| 10. Na Firauni mwenye majumba kama vigingi (Pyramids zilizoko Misri mpaka leo, nzima) | وَفِرْعَوْنَ ذِى الْأَوْتَادِ ۝١٠ |
| 11. Ambao walifanya maovu katika miji | الَّذِيْنَ طَغَوْا فِى الْبِلَادِ ۝١١ |

---

2. "Masiku" ni wingi wa "Usiku," na muradi hapa ni yale masiku kumi matukufu ya kumi la mwanzo la mwezi wa Dhulhijja, yaani tokea mwezi mosi mpaka mwezi kumi; na haya ndiyo masiku matukufu kuliko masiku yote hata Ramadhani pia, isipokuwa Usiku wa *Lailatul-Kadr* na masiku ya kumi la mwisho la huu mwezi wa Ramadhani. Basi na masiku haya pia ni muradi wake.

3. "Shaf-i" ni hisabu iwezayo kugawanyika kwa mbili (even number), na "witri" ni kila isiyoweza kugawanyika kwa mbili (odd number). Na makusudio ya Mwenyezi Mungu hapa ni kuapa kwa vitu vyote Alivyoviumba, vihisabikavyo kwa hisabu hii au hii.

7. Adi Iram ni kaumu ya Nabii Hudi; nao walikuwa wakubwa wana na nguvu sana, hata wakisema "Ni nani mwenye nguvu kuliko sisi!"

9. Thamudi ni kaumu ya Nabii Salih. Nao walikuwa wakikaa kaskazini ya Bara Arabu.

12. Kisha walizidisha humo mambo maovu?

فَأَكْثَرُوا فِيهَا الْفَسَادَ ﴿١٢﴾

13. Kwa hivyo Mola wako Aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu

فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٣﴾

14. Hakika Mola wako yuko katika malindizo!

إِنَّ رَبَّكَ لَبِالْمِرْصَادِ ﴿١٤﴾

15. Lakini mwanaadamu, Mola wake Anapomfanyia mtihani Akamtukuza na kumneemesha, basi husema: "Mola wangu amenitukuza;" (wala hashughuliki kufanya mema ili kutengeneza Akhera yake).

فَأَمَّا الْإِنْسَانُ إِذَا مَا ابْتَلَاهُ رَبُّهُ فَأَكْرَمَهُ وَنَعَّمَهُ
فَيَقُولُ رَبِّي أَكْرَمَنِ ﴿١٥﴾

16. Na Anapomfanyia mtihani Akampunguzia riziki yake, husema: "Mola Wangu Amenidhalilisha, (nikifanya mema au mabaya ni sawa sawa, hatayashughlikia, basi naendelea kufanya mabaya)".

وَأَمَّا إِذَا مَا ابْتَلَاهُ فَقَدَرَ عَلَيْهِ رِزْقَهُ فَيَقُولُ رَبِّي
أَهَانَنِ ﴿١٦﴾

17. Sivyo hivyo (mnavyodhania)! Bali nyinyi (matajiri) hamuwatazami mayatima kwa jicho la huruma

كَلَّا بَلْ لَا تُكْرِمُونَ الْيَتِيمَ ﴿١٧﴾

18. Wala hamujihimizi (wala kuhimiza wengine) kulisha maskini

وَلَا تَحَاضُّونَ عَلَىٰ طَعَامِ الْمِسْكِينِ ﴿١٨﴾

19. Na mnakula urithi kwa ulaji wa pupa

وَتَأْكُلُونَ التُّرَاثَ أَكْلًا لَمًّا ﴿١٩﴾

20. Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi.

وَتُحِبُّونَ الْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿٢٠﴾

21. Sivyo hivyo. (Kumbukeni) itakapovunjwa ardhi vipande vipande

كَلَّا إِذَا دُكَّتِ الْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢١﴾

22. Na kufika (amri ya) Mola wako, na Malaika safu safu.

وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٢﴾

23. Basi Siku hiyo italetwa Jahanamu. Siku hiyo mwanaadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini?

وَجِيءَ يَوْمَئِذٍ بِجَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ الْإِنْسَانُ وَأَنَّىٰ
لَهُ الذِّكْرَىٰ ﴿٢٣﴾

24. Atasema: "Laiti ningalitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo)".

يَقُولُ يَا لَيْتَنِي قَدَّمْتُ لِحَيَاتِي ﴿٢٤﴾

---

12. Katika mambo maovu aliyofanya Firauni ni kudai Uungu na kuua vijana wa kiume bila haki, na kuwaadhibu Banii Israil.

14. "Malindizo" ni mahali pa kuotea na kupeleleza na muradi hapa ni kuwa Mwenyezi Mungu Anawatazama waja Wake kila wakati wala hawafanyi jambo lolote ila huliona na kulidhibiti, kama afanyavyo aliyeko mahali pa kuotea na kupeleleza.

19. Waarabu kabla ya kuingia katika Uislamu walikuwa hawawarithishi wanawake wala vijana wadogo mayatima, bali mafungu yao katika mirathi walikuwa wakiyala wao kwa namna walivyokuwa wakipenda.

23. Makusudio ya kuletwa Jahanamu ni kudhihirishiwa watu waovu wakaiona.

25. Basi Siku hiyo hataadhibu yoyote namna ya kuadhibu Kwake (Mwenyezi Mungu)

فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾

26. Wala hatafunga yoyote jinsi ya kufunga kwake (Mwenyezi Mungu).

وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٦﴾

27. Ewe nafsi yenye kutua!

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾

28. Rudi kwa Mola wako, hali ya kuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na (Mwenyezi Mungu) aridhike na wewe.

ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾

29. Basi ingia katika (kundi la) waja Wangu (wazuri)

فَٱدْخُلِى فِى عِبَٰدِى ﴿٢٩﴾

30. Uingie katika Pepo Yangu.

وَٱدْخُلِى جَنَّتِى ﴿٣٠﴾ ع

---

25-26. Yaani hapana mfano wa adhabu ya Mwenyezi Mungu atakayowaadhibu makafiri Siku ya Kiama wala hapana mfano wa kifungo Atakachowafunga!

27. "Nafsi yenye kutua" ni nafsi ya mwenye kuamini akatenda aliyoamrishwa, akawacha aliyokatazwa. Ndiyo nafsi itakayotua Siku ya Kiama, sababu haitakuwa na khofu ya jambo Siku hiyo wala huzuni.

28. Maana yake: nafsi hiyo iliyotua itaridhika na Mwenyezi Mungu Siku hiyo; na Mwenyezi Mungu Ataridhika nayo.

آياتها ٢٠ (٩٠) سُورَةُ البَلَدِ مَكِّيَّةٌ (٣٥) رُكُوعُهَا ١

*Ina Aya 20* *Ina Kara 1*

# SURATUL BALAD

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa mji huu (wa Makka)

لَا أُقْسِمُ بِهَٰذَا الْبَلَدِ ①

2. Nawe utashuka (utateremka) katika mji huu (ambao wamekutoa na utahalalishiwa)

وَأَنتَ حِلٌّ بِهَٰذَا الْبَلَدِ ②

3. (Na Naapa) kwa kila kilichozaa na kila kilichozaliwa

وَوَالِدٍ وَمَا وَلَدَ ③

4. Kuwa Tumemuumba Mwanaadamu katika tabu.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي كَبَدٍ ④

5. Je! Anadhani ya kuwa hakuna yoyote atakayeweza (kumtia mkononi)?

أَيَحْسَبُ أَن لَّن يَقْدِرَ عَلَيْهِ أَحَدٌ ⑤

6. Anasema; "Nimeharibu mali mengi (kwa ajili ya kuupinga Uislamu)."

يَقُولُ أَهْلَكْتُ مَالًا لُّبَدًا ⑥

7. Je! Anadhani ya kuwa hakuna yoyote amuonaye? (Mwenyezi Mungu anamuona Atamlipa)

أَيَحْسَبُ أَن لَّمْ يَرَهُ أَحَدٌ ⑦

---

2. Kuhalalishiwa ni kupewa ruhusa kufanya jambo lililokatazwa. Kama ijulikanavyo, Mwenyezi Mungu Amekataza kabisa watu kupigana au kuuana katika mji wa Makka, hata mwenye kuuliwa mtu wake pia hana ruhusa kuchukuwa kisasi ndani ya Makka; ni lazima uwe ni mji wa amani siku zote. Basi hapa Mwenyezi Mungu anampa bishara Mtume wake, pamoja na waadi kuwa atamuhalalishia kuwapiga makafiri katika mji huu. Na Mwenyezi Mungu Akatimiza waadi wake. Wakati makafiri wa Makka walipovunja ahadi iliyokuwa baina yao na Waislamu alikwenda Mtume na jeshi lake, akaingia Makka. Na ruhusa hii alipewa Mtume peke yake kwa kadiri ya muda mdogo tu ili kuitahirisha Al-Kaaba, na kuondoa uchafu wa masanamu. Na baada ya hapo hakukuwa na ruhusa tena kupigana ndani ya Makka.

4. Mwanaadamu ana tabu nyingi ambazo hawana hayawani wengine: Hapati chakula ila kwa tabu na mashaka makubwa, naye lazima ale. Hapati nguo ila kwa tabu kubwa zaidi, naye ni lazima avae. Hawezi kustahamili hari wala baridi. Hawezi kujitetea bila silaha. Mwenyezi Mungu Amemlazimisha mambo kadha wa kadha, pamoja na kumkataza mengi. Na kila alifanyalo linadhibitiwa, na Akhera atakwendahisabiwa kwa kila alilolifanya, kubwa au dogo. Na tukiyafuata yote hayahisabiki.

5. Maana yake: anadhani mwanaadamu kwamba hakuna anayeweza kumrudi kwa makosa yake?

6,7. Maneno haya wanaambiwa wale makafiri waliokuwa wakitoa mali katika kupiga vita Dini ya Uislamu na kutaka kumuua Mtume (s.a.w.). Kisha wakajisifu kwa kutumia mali mengi. Kadhalika anaingia kila mwenye kuishikia Dini kinyume na kutaka kuiharibu. Nawasidhani kuwa Mungu hawaoni au hajui dhamiri zao mbovu.

| | |
|---|---|
| 8. Je! Hatukumpa macho mawili? | أَلَمْ نَجْعَل لَّهُۥ عَيْنَيْنِ ﴿٨﴾ |
| 9. Na ulimi na midomo miwili? | وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ﴿٩﴾ |
| 10. Na Tukambainishia zote njia mbili — (iliyo njema na iliyo mbaya)? | وَهَدَيْنَٰهُ ٱلنَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾ |
| 11. Je! Ameukata huo mlima, (njia nzito ya kumfikisha Peponi) | فَلَا ٱقْتَحَمَ ٱلْعَقَبَةَ ﴿١١﴾ |
| 12. Na nini kitakachokujulisha huo mlima (njia ya kukufikisha Peponi)? | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا ٱلْعَقَبَةُ ﴿١٢﴾ |
| 13. (Kuukata mlima huo) ni kumpa mtumwa uungwana | فَكُّ رَقَبَةٍ ﴿١٣﴾ |
| 14. Au kumlisha siku ya njaa | أَوْ إِطْعَٰمٌ فِى يَوْمٍ ذِى مَسْغَبَةٍ ﴿١٤﴾ |
| 15. Yatima aliye jamaa (na asiyekuwa jamaa) | يَتِيمًا ذَا مَقْرَبَةٍ ﴿١٥﴾ |
| 16. Au maskini aliye hohe hahe. | أَوْ مِسْكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ ﴿١٦﴾ |
| 17. Kisha awe miongoni mwa walioamini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana. | ثُمَّ كَانَ مِنَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلْمَرْحَمَةِ ﴿١٧﴾ |
| 18. Hao ndio watu wa upande wa kheri. | أُو۟لَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلْمَيْمَنَةِ ﴿١٨﴾ |
| 19. Lakini waliokanusha Aya Zetu, hao ndio watu wa upande wa shari. | وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا هُمْ أَصْحَٰبُ ٱلْمَشْـَٔمَةِ ﴿١٩﴾ |
| 20. Moto uliofungiwa (kila upande) utakuwa juu yao. | عَلَيْهِمْ نَارٌ مُّؤْصَدَةٌۢ ﴿٢٠﴾ ع |

11. Yaani: mbona mwanaadamu hashukuru neema hizi, akatumia mali yake katika mambo ya kheri aliyoyataja Mwenyezi Mungu katika Aya zijazo. Na maana ya Mwenyezi Mungu kuita mambo haya "njia nzito" ni kuwa yote ni mambo yaliyofungamana na kutoa mali, na hakuna kheri iliyo nzito kama iliyofungamana na mali. Na ukitaka kumpima mtu kuwa ni Islamu wa kweli, mtazame mwendo wake katika mali. Usihadaike kwa kumuona na nyuradi nyingi na kusali sana na kufunga sana; hayo ni mepesi kuyafanya. Mambo ni kutoa pesa.

13. Watu watiao aibu Dini ya Kiislamu kwa utumwa nawatafadhali wainue macho yao watazame Aya hii, na nyingi mfano wake katika Qurani zinazopigania uhuru, afahamu kuwa Uislamu unapenda zaidi uhuru kuliko hao wanaojidai kupenda uhuru, na atafahamu kuwa utumwa haupendezi aslan katika Dini hii.

رُكُوْعُهَا ١ (٢٦) سُوْرَةُ الشَّمْسِ مَكِّيَّةٌ (٩١) اٰيَاتُهَا ١٥

Ina Aya 15 — Ina Kara 1

## SURATUSH SHAMS

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Naapa kwa jua na kwa muangaza wake — وَالشَّمْسِ وَضُحٰهَا ۝١

2. Na kwa mwezi unapoliandama — وَالْقَمَرِ اِذَا تَلٰهَا ۝٢

3. Na kwa mchana unapolidhihirisha — وَالنَّهَارِ اِذَا جَلّٰهَا ۝٣

4. Na kwa usiku unapolifunika — وَالَّيْلِ اِذَا يَغْشٰهَا ۝٤

5. Na kwa mbingu na kwa Aliyezijenga — وَالسَّمَآءِ وَمَا بَنٰهَا ۝٥

6. Na kwa ardhi na kwa Aliyeitandaza — وَالْاَرْضِ وَمَا طَحٰهَا ۝٦

7. Na kwa nafsi (roho) na Aliyeitengeneza — وَنَفْسٍ وَّمَا سَوّٰهَا ۝٧

8. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake — فَاَلْهَمَهَا فُجُوْرَهَا وَتَقْوٰهَا ۝٨

9. Bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake) — قَدْ اَفْلَحَ مَنْ زَكّٰهَا ۝٩

10. Na bila shaka amejihasiri aliyeiviza (nafsi yake). — وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسّٰهَا ۝١٠

11. Kina Thamudi walikadhibisha kwa sababu ya upotofu (upotevu) wao — كَذَّبَتْ ثَمُوْدُ بِطَغْوٰهَآ ۝١١

---

1-2. Wamegeuza muradi wa matamko yaliyomo katika Aya hizi walizozifanya ni ya 2 na 3. Wakasema Shams ni Nabii Muhammad (s.a.w.). Na hakuna mfasiri yoyote aliyefasiri hivi. Na wakasema Al-Qamar ni mtu wao. Huu ni uwongo na ukafiri ulio dhahiri.

9-10. Kuitikasa nafsi ni kuipamba kwa ilimu na amali njema. Na hayo ndiyo mambo yamkamilishayo mtu hata akafaa kuitwa "mtu", na ndio yamtukuzayo duniani na Akhera. Na kuiviza nafsi ni kuidharau ukaiwachilia mbali ikafuata ipendalo, hata ikaingia katika uchafu na maasia na ujinga, ikawa dhalili duniani na Akhera.

11. "Thamudi" wametangulia kutajwa katika Sura ya *Al-Buruuj* na Sura ya *Al Fajr*. Watu hawa walimtaka Mtume wao, Nabii Salih (a.s.), awatolee ngamia katika jabali ndipo watamsadiki kuwa ni Mtume kweli. Nabii Salih akaomba Mungu, likapasuka lile jabali akatoka ngamia kama walivyotaka, lakini pia wasiamini. Nabii Salih akawaambia "Tahadharini naye huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu, musimguse kwa madhara yoyote," na akawalazimisha kuwa siku moja wateke wao maji ya kuwatosha kwa siku mbili, na siku ya pili wamuachie yule ngamia peke yake, wao wasiteke. Wakamfanya ni muongo. Na mmoja aliyekuwa mshupavu zaidi katika wao, akenda akamchinja! Mwenyezi Mungu akawateremshia adhabu kwa sababu ya makosa hayo, ikawaenea wote, aliyemchinja ngamia na asiyemchinja pia. Hili linafahamisha kwamba watu wasipokanyana maovu, basi ikishuka adhabu ya Mwenyezi Mungu huwaenea wote; waliofanya makosa yale na wasiofanya.

إِذِ انبَعَثَ أَشْقَاهَا ﴿١٢﴾

12. Aliposimama muovu wao mkubwa (ili kumchinja huyo ngamia wa miujiza)

فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ اللَّهِ نَاقَةَ اللَّهِ وَسُقْيَاهَا ﴿١٣﴾

13. Hapo Mtume wa Mungu aliwaambia: "(Huyu) ni ngamia wa Mwenyezi Mungu, (muacheni) na kinywaji chake, (msimzuilie maji wala msimuue)".

فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُم
بِذَنبِهِمْ فَسَوَّاهَا ﴿١٤﴾

14. Lakini walimkadhibisha (huyo Mtume, Nabii Salih) na wakamuua (huyo ngamia); kwa hivyo Mola wao Aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na akawafuta kabisa

وَلَا يَخَافُ عُقْبَاهَا ﴿١٥﴾

15. Wala Haogopi matokeo yake.

---

15. Mtu akitaka kufanya jambo lolote kwanza inataka kuzingatia mwisho wake, ukiwa mzuri alifanye; na ukiwa ni muovu aliwache. Lakini Mwenyezi Mungu anaweza atakalo sababu Yeye hana Alichelealo kumfikia au kumpungukia au kumharibikia. Na Hafanyi ila yaliyo ndiyo tu.

آياتها ٢١ سُورَةُ اللَّيْلِ مَكِّيَّةٌ (٩٢) (٩) ركوعها ١

*Ina Aya 21* **SURATUL LAYL** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa usiku ufunikapo (kila kitu)

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰ ﴿١﴾

2. Na kwa mchana uangazapo

وَالنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ﴿٢﴾

3. Na kwa Aliyeumba kiume na kike

وَمَا خَلَقَ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٣﴾

4. Kuwa amali zenu ni mbali mbali; (na jaza yenu itakuwa mbali mbali).

إِنَّ سَعْيَكُمْ لَشَتَّىٰ ﴿٤﴾

5. Yule anayetoa (zaka, sadaka na vingenevyo) na kumcha Mwenyezi Mungu

فَأَمَّا مَنْ أَعْطَىٰ وَاتَّقَىٰ ﴿٥﴾

6. Na kusadiki jambo jema (akalifuata)

وَصَدَّقَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿٦﴾

7. Tutamsahilishia njia ya kwenda Peponi.

فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْيُسْرَىٰ ﴿٧﴾

8. Na afanyaye ubakhili, asiwe na haja ya viumbe wenzake

وَأَمَّا مَن بَخِلَ وَاسْتَغْنَىٰ ﴿٨﴾

9. Na akakadhibisha mambo mema (asiyafanye)

وَكَذَّبَ بِالْحُسْنَىٰ ﴿٩﴾

10. Tutamsahilishia njia ya kwendea Motoni.

فَسَنُيَسِّرُهُ لِلْعُسْرَىٰ ﴿١٠﴾

11. Na mali yake hayatamfaa atakapokuwa anadidimia (Motoni humo).

وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّىٰ ﴿١١﴾

12. Ni juu yetu (kuwabainishia viumbe) njia ya kheri na njia ya shari.

إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَىٰ ﴿١٢﴾

13. Na ni Yetu sisi Akhera na dunia.

وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ ﴿١٣﴾

14. Basi nakuhadharisheni na Moto uwakao (kwa nguvu).

فَأَنذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّىٰ ﴿١٤﴾

---

4. Maana yake katika watu kuna wafanyao mema na wafanyao maovu, kuna wafanyao amali za Akhera na watumikiao ulimwengu, kuna wafanyao yaliyo na faida na yaliyo na madhara.

5. Makusudio ni kutoa mali na nafsi pia. Yaani atumie mali yake katika kutekeleza haki za Mwenyezi Mungu na viumbe wenziwe, na atumie nafsi yake vile vile.

6. Maana ya "kusadiki jambo jema".ni kushikamana na kila alililoamrisha Mwenyezi Mungu, sababu Yeye haamrishi ila jema wala hakatazi ila ovu.

7. Maana yake: Tutamsahilishia njia ya kufanya mambo mema hata awe haoni raha ila katika kumtii Mwenyezi Mungu na kufanya kheri.

| | |
|---|---|
| 15. Hatauingia ila muovu | لَا يَصْلَىٰهَآ إِلَّا ٱلْأَشْقَى ﴿١٥﴾ |
| 16. Anayekadhibisha na kuipa mgongo (hii dini ya haki). | ٱلَّذِى كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٦﴾ |
| 17. Na amchaye (Mwenyezi Mungu) ataepushwa nao. | وَسَيُجَنَّبُهَا ٱلْأَتْقَى ﴿١٧﴾ |
| 18. Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa | ٱلَّذِى يُؤْتِى مَالَهُۥ يَتَزَكَّىٰ ﴿١٨﴾ |
| 19. Na hali ya kuwa hakuna yoyote aliyemfanyia ihsani ili awe anamlipa | وَمَا لِأَحَدٍ عِندَهُۥ مِن نِّعْمَةٍ تُجْزَىٰٓ ﴿١٩﴾ |
| 20. Isipokuwa (anafanya haya) kwa kutaka radhi ya Mola wake Mtukufu. | إِلَّا ٱبْتِغَآءَ وَجْهِ رَبِّهِ ٱلْأَعْلَىٰ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Basi atapata la kumridhisha. | وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ﴿٢١﴾ |

---

18. Mapendeleo ni kujitakasa nafsi yake na dhambi za kuzuia haki za Mwenyezi Mungu na kutakasa mali yake na haki za maskini. Sababu mtu akiwa hatoi Zaka, mali yake huwa yametangamana na haki za maskini, na atakapoyatumia huwa anatumia mali yake na ya watu, wala hayatahiriki mpaka atoe Zaka. Na haki za Mwenyezi Mungu ni kutoa mali katika kunusuru Dini Yake kwa kila iwezekanavyo, na kusaidia kila wahitaji, si kutoa Zaka tu, kama wanavyoodhania watu wengine.

19-20. Maana ya Aya mbili hizi Mtu huyu hatoi mali yake kwa sababu ya kulipa ihsani ya mtu, bali anatoa kwa sababu ya kutaka Radhi ya Mola wake tu.

21. Yaani Mwenyezi Mungu Atamridhisha kwa Malipo mema, mpaka aridhie. Aya hizi tangu 17 zimeshuka kwa sababu ya Sayyidna Abubakr (r.a.) aliyekuwa akitoa mali yake katika kununua watumwa waliokuwa wakiadhibishwa na bwana zao kwa sababu ya kusilimu, kisha akiwawacha huru. Na mmoja katika hao ni Sayyidna Bilali, muadhini wa Mtume. Na kadhalika zinamhusu kila atakayetumia mali yake katika kunusuru dini.

اياتها ١١ (٩٣) سورة الضحى مكية (١١) ركوعها ١

*Ina Aya 11* | **SURATUDH DHUHAA** | *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa mchana

وَالضُّحَىٰ ①

2. Na kwa usiku unapotanda

وَاللَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ②

3. Hakukuacha Mola wako wala hakukasirika (nawe Ewe Nabii Muhammad).

مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ③

4. Na bila shaka (kila) wakati ujao (utakuwa) ni bora kwako kuliko uliotangulia.

وَلَلْآخِرَةُ خَيْرٌ لَكَ مِنَ الْأُولَىٰ ④

5. Na Mola wako Atakupa mpaka uridhike.

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ⑤

6. Je! Hakukukuta yatima akakupa makazi (mazuri ya kukaa)?

أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَآوَىٰ ⑥

7. Na Akakukuta hujui kuongoza njia, akakuongoza?

وَوَجَدَكَ ضَالًّا فَهَدَىٰ ⑦

8. Na Akakukuta fakiri Akakutajirisha?

وَوَجَدَكَ عَائِلًا فَأَغْنَىٰ ⑧

---

3. Katika siku za mwanzo mwanzo wa kudhihiria Uislamu, zilipita siku ambazo Mtume (s.a.w.) hakuteremshiwa Wahyi. Mtume akafanya wasiwasi na huzuni kubwa, na wale makafiri wa Makka wakawa humfanyia stihizai, wakimwambia "Jee, Mola wako amekutupa au amekukasirikia?" Basi hapa Mwenyezi Mungu anamliwaza Mtume wake, pamoja na kuwajibu wale makafiri kwamba hakumuwacha wala hakukasirika naye.

4. Aya hii yaishiria kwamba kila siku zijazo Mtume atakwendelea juu kuliko siku zilizopita, na ndivyo alivyokuwa; kila siku alikuwa akiendelea juu. Na ndivyo ilivyo mpaka sasa. Kila siku dini yake inazidi kutangaa na yeye kuzidi daraja.

5. Vipewa (atiya) hivi alivyoahidiwa Mtume na Mola Wake vyakusanya vipewa vya duniani na Akhera. Duniani alimpa kila alilokuwa akilitamani, kama kumuongolea uma wake, na kuitukuza dini yake na kuwashinda maadui zake. Na yote hayo Mungu akamfanyia kwa muda mchache wa kustaajabisha. Na vipewa vya Akhera alivyomuandalia havina hisabu wala hakuna avijuae ila Yeye Mwenyewe tu *Subhanahuu wa Taala*.

8. Katika aya hii na mbili zilizo kabla yake, Mwenyezi Mungu anamkumbusha Mtume Wake neema Zake kubwa Alizotangulia kumneemesha. Anafanya haya kwa njia ya kumliwaza. Mtume (s.a.w.) alizaliwa baada ya kufa baba yake, akawa yatima. Na dasturi ya kijana akiwa yatima hupata tabu, na ghalibu hupotea akiwa kati ya watu wajinga kama hao makafiri wa Makka. Lakini Mwenyezi Mungu kwa Rehema yake, akamhifadhi na kila tabu na kila upotevu. Akakulia katika umaskini, hata akawahi kuchunga mbuzi ili kumsaidia ami yake. Mwenyezi Mungu akamtajirisha kwa kumtia mahaba bibi tajiri kabisa (Mwana Khadija) akataka Mtume amuowe; akamuowa. Alikuwa akiwaona jamaa zake wakiabudu masanamu waliokuwa wakiwafinyanga wao wenyewe kwa mikono yao; akajuwa kuwa wamepotea, lakini hajuwi awaongowe namna gani. Akawa amedangana na kupigwa na mshangao, hajuwi la kufanya. Hata mwisho akawa haoni raha tena kukaa ndani ya mji, akahamia majabalini ili apate faragha ya kuzidi kufikiri, na kumuomba Mungu amuoneshe njia iliyo sawa. Mwenyezi Mungu akamuonesha njia ya uongofu ya kuongoka yeye na jamaa zake.

9. Basi usimuonee yatima.

فَأَمَّا الْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ﴿٩﴾

10. Wala usimkaripie aulizaye.

وَأَمَّا السَّائِلَ فَلَا تَنْهَرْ ﴿١٠﴾

11. Na neema ya Mola wako isimulie (kwa kushukuru na kwa kufanya amali njema).

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

---

9-10. Aya hizi maana yake ni haya: Kama ambavyo Mwenyezi Mungu Alikukuta wewe yatima, akakuhifadhi, basi nawe mhifadhi kila yatima, usimdhalilishe. Na kama Alivyokukuta wewe umedangana hujui njia ya uwongofu. Naye akakuongowa, basi na wewe muoneshe njia ya uwongofu kila atakayekuja kuuliza, usimkaripie; (usimtolee ukali).

11. Maana: Izungumze kwa njia ya kushukuru; si kwa njia ya kujisifu.

ركوعها ١ (١٢) سُورَةُ أَلَمْ نَشْرَحْ مَكِّيَّةٌ (٩٤) اٰيَاتُهَا ٨

Ina Aya 8 — Ina Kara 1

## SURATU ALAM-NASHRAH

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Je! Hatukukupanulia kifua chako

أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ①

2. Na tukakuondolea mzigo wako (mzito)

وَوَضَعْنَا عَنْكَ وِزْرَكَ ②

3. Uliovunja mgongo wako (yaani hatukukuondoshea mambo yako mazito mazito)

الَّذِيْٓ أَنْقَضَ ظَهْرَكَ ③

4. Na tukakutukuza utajo wako.

وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ④

5. Basi kwa hakika pamoja na dhiki (huja) faraji

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ⑤

6. Hakika pamoja na dhiki (huja) faraji.

إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ⑥

7. Basi ukishamaliza (kulingania) shughulika (kwa ibada)

فَإِذَا فَرَغْتَ فَانْصَبْ ⑦

8. Na jipendekeze kwa Mola wako.

وَإِلٰى رَبِّكَ فَارْغَبْ ⑧ ع ١٩

---

1. Kupanuliwa kifua ni kuondolewa shaka na wasiwasi na kama haya.

2. Maana ya "mzigo" hapa ni ile hamu kubwa aliyokuwa nayo kabla ya kupewa Utume, ya kuwaona watu katika upotevu naye akawa hajui namna ya kuwaongowa.

4. Mwenyezi Mungu ameutukuza utajo wa Bwana wetu Muhammad (s.a.w.) kwa kumpa Utume, na kumfanya bora kuliko Mitume yote, na dini yake akaifanya ndiyo ya mwisho isiyofutwa na dini ya Mtume mwengine na ndio bora kuliko dini zote zilizotangulia, kwa kuwa ndiyo dini peke yake inayoweza kuwafaa watu wa jinsi yoyote, katika zama zozote, na mahali popote.

6. Hii ni bishara ya kuwa baada ya tabu iliyokuwa ikimpata Mtume kwa Makafiri, itakuja Faraji ya Mwenyezi Mungu, amnusuru juu ya maadui zake.

7. Maana yake: Ukisha kazi yako ya kuwafikilizia watu uliyotumwa na Mwenyezi Mungu, fanya ibada nyingi umshukuru Mola wako kwa neema zake alizokuneemesha. Na Mtume (s.a.w.) alikuwa akijipa tabu sana katika ibada, akawa husimama katika Sala hata miguu yake ikafilia damu, na akisujudu hata akadhaniwa amekufa! Na katika Saumu alikuwa akifunga siku kadha wa kadha pasi na kula kitu mchana wala usiku; lakini aliwataka Masahaba wasimfuwate, kwa hivyo si vizuri kwa asiyekuwa yeye kufanya hivi.

آياتها ٨ (٩٥) سورة التين مكية (٢٨) ركوعها ١

*Ina Aya 8* **SURATUT TYN** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa Tini na Zaytuni. (Chini ya miti hii amepata Utume Nabii Ibrahimu na Nabii Nuhu)

وَالتِّينِ وَالزَّيْتُونِ ﴿١﴾

2. Na kwa mlima Sinai. (Amepata Kitabu hapo Nabii Musa)

وَطُورِ سِينِينَ ﴿٢﴾

3. Na kwa mji huu wenye amani, (Makka alipopelekewa Utume Nabii Muhammad)

وَهَٰذَا الْبَلَدِ الْأَمِينِ ﴿٣﴾

4. Bila shaka Tumemuumba mwanaadamu kwa umbo lililo bora kabisa.

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾

5. Halafu Tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini

ثُمَّ رَدَدْنَاهُ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٥﴾

6. Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha, (unaondelea maisha).

إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦﴾

7. Basi ni lipi likupalo, kukadhibisha malipo baada (ya kuona hayo)?

فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعْدُ بِالدِّينِ ﴿٧﴾

8. Je! Mwenyezi Mungu si Hakimu muadilifu kuliko mahakimu wote? (Basi si lazima atawalipa kwa mema yao na wabaya kwa mabaya yao)?

أَلَيْسَ اللَّهُ بِأَحْكَمِ الْحَاكِمِينَ ﴿٨﴾

---

4. Kàtika hayawani wote hakuna kama mwanadamu kwa umbo na akili.

5. Mwanaadamu ana hali mbili: Akitumia akili yake huongoka akawa bora kuliko hayawani wengine; na asipotumia akili yake hupotea na hayawani wengine wote wakawa bora kuliko yeye na huko ndiko kuwa "chini kuliko walio chini".

7-8. Mwenyezi Mungu anamwambia mwanaadamu: Baada ya kujua kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kufanya kama hayo, ni lipi tena likupalo kukadhibisha malipo ya siku ya Kiama? Hujajua kwamba Mwenye kufanya yote hayo hapana shaka kwamba amefanya mambo Yake yote kwa umadhubuti sana, wala hapana liwezalo kumharibikia au kumshinda?

اٰيَاتُهَا ١٩ (٩٦) سُوْرَةُ الْعَلَقِ مَكِّيَّةٌ (١) رُكُوْعُهَا

Inu Aya 19

## SURATUL ALAQ

*(Imeteremka Makka)*

Ina Kara 1

Kwajina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba

اِقْرَاْ بِاسْمِ رَبِّكَ الَّذِيْ خَلَقَ ۝١

2. Amemuumba mwanaadamu kwa pande la damu.

خَلَقَ الْاِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ۝٢

3. Soma, na Mola wako ni Karimu sana

اِقْرَاْ وَرَبُّكَ الْاَكْرَمُ ۝٣

4. Ambaye Amemfundisha (Binadamu ilimu zote hizi) kwa wasita (msaada) wa kalamu; (zilizoandika vitabu, watu wakapata ilimu)

الَّذِيْ عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ۝٤

5. Amemfundisha mwanaadamu (chungu ya) mambo aliyokuwa hayajui.

عَلَّمَ الْاِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ۝٥

6. Sivyo hivi (we Binadamu)! Kwa hakika binadamu hutakabari

كَلَّآ اِنَّ الْاِنْسَانَ لَيَطْغٰىٓ ۝٦

7. Akijiona amepata utajiri!

اَنْ رَّاٰهُ اسْتَغْنٰى ۝٧

8. Bila shaka marejeo (ya wote) ni kwa Mola wako (tu).

اِنَّ اِلٰى رَبِّكَ الرُّجْعٰى ۝٨

9. Je! Umemuona yule anayemkataza

اَرَءَيْتَ الَّذِيْ يَنْهٰى ۝٩

---

1. Tumetangulia kusema katika Sura ya *Adh-Dhuhaa,* maelezo ya Aya 8, Bwana wetu Muhammad (s.a.w.) kabla ya kupewa Utume alikuwa na huzuni na wasiwasi mwingi kwa kuwaona jamaa zake katika upotevu, naye hajui namna ya kuwaongoa. Mwisho akahamia majabalini karibu ya Makka, akawa anaabudu na kufikiri, na kuomba Mwenyezi Mungu amuoneshe njia ya uongofu. Basi siku moja alipokuwa katika pango la jabali la Hiraai, karibu ya Makka, katika kuabudu, mara alimtokea Malaika, akamwita "Ewe Muhammad! Mimi ni Jibrili na wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe!" Kisha akamwambia "Soma!" Mtume akamjibu "Mimi si msomaji." (maana sijui kusoma). Jibrili akamshika Mtume akamminya kwa nguvu, hata Mtume akaona tabu. Kisha akamuacha, akamwambia tena "Soma!" Mtume akamjibu vile vile, naye akamfanyia tena kama mara ya kwanza. Hata mara ya tatu ndipo alipomsomea Aya hizi tangu Aya 1 mpaka 5. Na Aya hizi ndizo za kwanza kushuka katika Qurani.

2. Manii, baada ya kukaa siku arubaini katika uzao, hugeuka pande la damu, ndio makusudio ya hapa.

3. Aya hii mpaka Aya ya 5, kama kwamba ajibiwa Mtume (s.a.w.) kwa kule kusema "mimi si msomaji". Basi Mwenyezi Mungu anamwambia kuwa Yeye ni Karimu mno, na Ndiye aliyewafunza watu, kwa wasita wa kalamu, yote waliyokuwa hawajui. Basi kwa Ukarimu wake mkubwa na Uwezo wake wa kufanya kila alitakalo, si uzito kwake kumfunza Mtume Wake kusoma.

8. Maana yake Usighurike kwa hayo mali, kwani huna budi utarejea kwa Mola wako, na mali yako hayatakufaa kitu mbele zake.

9. Aliyekusudiwa kwa Aya hizi 9-19 ni Abu-Jahl, adui mkubwa wa Mtume (s.a.w.) aliposema "Nikimuona Muhammad anasali nitamkanyaga shingo yake!"

10. Mja (wa Mungu) akisali?

عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰ ⑩

11. Je! Umeona kama yeye yuko juu ya uwongofu (kwa kufanya hivyo)?

أَرَأَيْتَ إِن كَانَ عَلَى الْهُدَىٰ ⑪

12. Au anaamrisha wema (kwa kufanya hivyo, au anafanya mabaya)?

أَوْ أَمَرَ بِالتَّقْوَىٰ ⑫

13. Je unaonaje! Kama yeye anakadhibisha na kurudi nyuma?

أَرَأَيْتَ إِن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ⑬

14. Je! Hajui ya kuwa Mwenyezi Mungu Anamuona?

أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ اللَّهَ يَرَىٰ ⑭

15. Sivyo hivyo (anavyofanya!) Kama haachi, Tutamkokota kwa nywele za utosi (wake tumtie Motoni) —

كَلَّا لَئِن لَّمْ يَنتَهِ لَنَسْفَعًا بِالنَّاصِيَةِ ⑮

16. Utosi muongo, wenye madhambi.

نَاصِيَةٍ كَاذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ⑯

17. Basi na awaite wanachama wenzake (wamsaidie)

فَلْيَدْعُ نَادِيَهُ ⑰

18. Na sisi Tutawaita Malaika wa Motoni (wamuadhibu) —

سَنَدْعُ الزَّبَانِيَةَ ⑱

19. Sivyo! Usimtii (mbaya huyo), bali sujudu na uwe karibu (na Mungu wako).

كَلَّا لَا تُطِعْهُ وَاسْجُدْ وَاقْتَرِبْ ۩ ⑲

---

Na maana ya Aya hizi 9-14 ni haya: Umemuona mtu mbaya huyu? Ambaye humkataza mja wa Mwenyezi Mungu kusali, na hali huyo mwenye kukatazwa yumo katika uongofu na kuamrisha mema; na huyo mwenye kukataza anakadhibisha dini na kuipa mgongo? Hajui kama Mwenyezi Mungu anamuona wala hatamuacha?

Siku moja Abu-Jahl alimuona Mtume akisali, akataka kutimiza maneno yake, akamwendea kutaka kumkanyaga shingo. Kabla hajamfikilia akaona handaki ya moto baina yake yeye na Mtume; akarudi mbio.

15. Makusudio ya "nywele" hapa ni huyo mwenye nywele.

18. Hii ni jawabu ya Abu-Jahl, wakati Mtume alipomkemea kwa kutaka kumzuilia kusali. Alisema "Unajuwa kama hapa Makka hapana mtu mwenye watu wengi kama mimi; nikitaka nitakujazia jeshi katika wangwa huu (yaani wampige vita Mtume). "Zabaniya" ni Malaika amewaumba Mwenyezi Mungu ili kuwaadhibu watu waovu katika Jahanamu.

آياتها ٥ (٩٧) سُورَةُ الْقَدْرِ مَكِّيَّة (٢٥) ركوعها ١

*Ina Aya 5*

# SURATUL QADR

*Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

إِنَّا أَنزَلْنَاهُ فِي لَيْلَةِ الْقَدْرِ ﴿١﴾

1. Hakika Tumeiteremsha (Qurani) katika Laylatul-Qadr (usiku wenye hishima kubwa), (usiku wa mwezi wa Ramadhani).

وَمَا أَدْرَاكَ مَا لَيْلَةُ الْقَدْرِ ﴿٢﴾

2. Na jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) ni nini huo usiku wa Laylatul-Qadr?

لَيْلَةُ الْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٣﴾

3. Huo usiku wa hishima (huo) ni bora kuliko miezi elfu.

تَنَزَّلُ الْمَلَائِكَةُ وَالرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِم مِّن كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾

4. Huteremka Malaika na roho (za viumbe watakatifu) katika (usiku) huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo

سَلَامٌ هِيَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ الْفَجْرِ ﴿٥﴾

5. Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya alfajiri.

---

1. Qurani—kama ijulikanavyo — ilikuwa ikiteremshwa kidogo kidogo, basi siku ile iliyoanza kuteremshwa ilikuwa katika *Laylatul-Qadr* (usiku wenye hishima kubwa). Ndio ikaambiwa kuwa Qurani imetermshwa katika *Laylatul-Qadr*, ni usiku mmoja mtukufu umo katika mwezi wa Ramadhani, ambao umebarikiwa kuliko mezi alfu; yaani mtu akifanya amali njema katika usiku huo hupata thawabu kama za mwenye kufanya amali ile kwa zaidi ya mezi elfu: na mwenye kufanya maovu naye hupata dhambi za mwenye kufanya maovu kama yale kwa zaidi ya miezi alfu. Na Mwenyezi Mungu ameuficha usiku huu haujulikani ni upi, ili watu wajitahidi kufanya ibada katika mwezi mzima wa Ramadhani; lakini watarajiwa zaidi kuwa katika kumi la mwisho na khasa usiku wa kuamkia mwezi 23,25,27 na 29. Basi atakaye kujua yakini kuwa ameupata usiku huu, bila ya shaka, inamlazimu ajipinde na kufanya ibada mwezi mzima. Wala si lazima kwa mwenye kuupata usiku huu kuona alama yoyote.

4. Yaani kwa ajili ya mambo aliyoyakadiri Mwenyezi Mungu katika mwaka ule.

5. Amesema Baidhawy katika maana ya Aya hii: Katika usiku huu Mungu hakadiri ila amani tupu; na katika masiku mengine hukadiriwa amani na balaa.

آياتها ٨ (٩٨) سُورَةُ الْبَيِّنَةِ مَدَنِيَّةٌ (١٠٠) رُكُوعُهَا ١

*Ina Aya 8* *Ina Karu 1*

# SURATUL BAYYINAH

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa, na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Wale waliokufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na washirikina (walitoa ahadi kuwa) hawataacha (waliyonayo) mpaka iwajie hoja (iliyo dhahiri ya kuonesha upotofu wa dini yao hiyo)

لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنفَكِّينَ حَتَّىٰ تَأْتِيَهُمُ الْبَيِّنَةُ ①

2. (Naye ni) Mtume aliyetoka kwa Mwenyezi Mungu anayewasomea kurasa zenye kutakaswa

رَسُولٌ مِّنَ اللَّهِ يَتْلُو صُحُفًا مُّطَهَّرَةً ②

3. Ndani yake humo zimo Sharia madhubuti.

فِيهَا كُتُبٌ قَيِّمَةٌ ③

4. Wala hawakutengukana (hawakufarikiana) wale waliopewa Kitabu ila baada ya kuwajia hoja hiyo (waliyokuwa wakiitaka).

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَةُ ④

5. Wala hawakuamrishwa ila kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia dini, wawache dini za upotofu, (upotevu) na wasimamishe Sala na kutoa Zaka — hiyo ndiyo dini iliyo sawa. (Nao wameikataa).

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ ۚ وَذَٰلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ ⑤

---

1. Makafiri waliopewa Kitabu ni Mayahudi na Wamasihia: na "Washirikina" ni wale wanaoabudu masanamu. Na muradi wa Aya hizi 1-4 ni kwamba kabla ya kudhihiri Mtume (s.a.w.) Mayahudi na wamasihia waliokuwa Madina, walipokuwa wakipigana na wale washirikina, walikuwa wakiwaambia "Karibu atadhihiri Mtume, na sisi tutamfuwata tuwe pamoja naye, tukupigeni nyinyi." Na walikuwa wakitaraji kuwa Mtume huyo atakuwa katika wao. Wale washirikina walipokuwa wakisikia maneno haya waliathirika, wakawa nao pia wanamngojea huyo Mtume; ndio maana ya kuwa wote taifa tatu "hawataacha (waliyonayo) mpaka iwajie hoja." Maana kila taifa katika tatu hizi ilikuwa na azma ya kushikamana na mila yao, wasiwache mpaka ije hoja. Na makusudio ya hoja hapa ni Mtume, kama ilivyobaini Aya ya pili. Hata alipokuja Mtume wale washirikina wakamuamini mbele; ama Mayahudi na Wamasihia, walipomuona Mtume si katika wao kama waliyyokuwa wakitaraji, wakatengukana; baadhi yao wakamuamini, na baadhi wasimuamini, ndiyo maana ya kuwa "hawakutengukana waliopewa Kitabu ila baada ya kuwajilia wao Hoja."

2. Mapendeleo ya madaftari yenye kutakasiwa ni Qurani.

3. Au maana yake "ndani yake muna vitabu vilivyo sawa." Na ni kuwa katika Qurani muna VIINI vya mafundisho ya Vitabu vya Mwenyezi Mungu vilivyotangulia.

5. Maana yake: Mtume huyu hakuwajilia na jambo jipya kama watamkadhibisha, bali analowaamrisha yeye ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia ibada, na kusimamisha Sala, na kutoa Zaka, haya haya ndiyo waliyoamrishwa wafuasi wa dini zote zilizo sawa zilizotoka kwa Mwenyezi Mungu, ambazo wao wazikubali.

6. Bila shaka wale waliokufuru miongoni mwa watu waliopewa Kitabu na washirikina wataingia katika Moto wa Jahanamu, wakae humo milele; hao ni waovu wa viumbe.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتٰبِ وَالْمُشْرِكِينَ فِي نَارِ جَهَنَّمَ
خٰلِدِينَ فِيهَا ۚ أُولٰٓئِكَ هُمْ شَرُّ الْبَرِيَّةِ ۝٦

7. Hakika wale walioamini na kutenda mema, basi hao ndio wema wa viumbe.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ ۙ أُولٰٓئِكَ هُمْ خَيْرُ
الْبَرِيَّةِ ۝٧

8. Malipo yao kwa Mola wao ni mabustani ya daima ambayo mito inapita mbele yake, wakae humo milele; Mwenyezi Mungu Amewaridhia, nao wameridhika. (Malipo) hayo ni kwa yule anayemuogopa Mola wake.

جَزَآؤُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنّٰتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهٰرُ
خٰلِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ رَضِيَ اللّٰهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۚ
ذٰلِكَ لِمَنْ خَشِيَ رَبَّهُ ۝٨ ع

اٰيَاتُهَا ٨ (٩٩) سُوْرَةُ الزِّلْزَالِ مَدَنِيَّةٌ (٩٣) رُكُوْعُهَا ١

Ina Aya 8

# SURATUZ ZILZAL

Ina Kara 1

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Itakapotetemeshwa ardhi mtetemesho wake (huo mkubwa)

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴿١﴾

2. Na itakapotoa ardhi mizigo yake (hiyo)

وَأَخْرَجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ﴿٢﴾

3. Na binadamu akasema (wakati huo): "(Oh!) Ina nini (leo ardhi)?"

وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا لَهَا ﴿٣﴾

4. Siku hiyo itatoa habari zake (zote).

يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿٤﴾

5. Kwa kuwa Mola wake Ameifunulia (ameiamrisha kufanya hayo).

بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ﴿٥﴾

6. Siku hiyo watu watatoka (makaburini) vikundi - vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao.

يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا لِيُرَوْا أَعْمَالَهُمْ ﴿٦﴾

7. Basi anayefanya wema (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾

8. Na anayefanya uovu (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake.

وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾

---

2. Wamirzai wameona kuwa Aya hizo zimehusiana na Kiama; wao wanasema kuwa mizigo yake ni maadini na ilimu . . .

4. Namna itakavyotoa habari ama ni kwa kutamshwa na Mwenyezi Mungu, kama atakavyovitamsha vitu kadha-wa-kadha visivyotamka, au ni kuwa ile hali ya ardhi itakavyokuwa, itatosha kumfahamisha mtu pasi na ardhi kutamka; kama tuwezavyo kumtambua mwenye furaha na mwenye hasira na mwenye njaa na mwenye shibe, pasi na kutamka. Na habari itakayotoa ardhi siku hiyo ni hii: Amesema Mtume (s.a.w.) "Siku ya Kiama ardhi itamshuhudilia kila mtu na kila umma, alilolifanya juu yake" (YAANI JUU YA ARDHI). Na haya ndiyo mapendeleo ya ardhi "kutoa habari zake".

7-8. Na Aya mbili hizi zafahamisha kwamba mwanaadamu atajaziwa kwa kila alitendalo, la kheri au la shari hata likiwa dogo sana kama uzani wa chungu mdogo pia.

ركوعها ١ (١٤) سورة العديت مكية (١٠٠) اياتها ١١

Ina Aya 11

# SURATUL AADIYAT

Ina Kara 1

*(Imeteremka Makka)*

| | |
|---|---|
| Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo. | بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ |
| 1. Naapa kwa (farasi) wanaokwenda mbio wakihema | وَالْعٰدِيٰتِ ضَبْحًا ① |
| 2. Na wakitoa moto kwa kupiga kwato (zao chini) | فَالْمُوْرِيٰتِ قَدْحًا ② |
| 3. Wakashambulia wakati wa asubuhi | فَالْمُغِيْرٰتِ صُبْحًا ③ |
| 4. Wakarusha mavumbi (makubwa) wakati huo | فَاَثَرْنَ بِهٖ نَقْعًا ④ |
| 5. Na wakaingia kati ya kundi (la maadui wakapigana) | فَوَسَطْنَ بِهٖ جَمْعًا ⑤ |
| 6. (Naapa kwa haya nasema kuwa): Bila shaka Mwanaadamu amkanusha Mola wake. | اِنَّ الْاِنْسَانَ لِرَبِّهٖ لَكَنُوْدٌ ⑥ |
| 7. Naye anayajua haya. | وَاِنَّهٗ عَلٰى ذٰلِكَ لَشَهِيْدٌ ⑦ |
| 8. Na ana mapenzi makubwa kabisa ya kupenda mali. | وَاِنَّهٗ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيْدٌ ⑧ |
| 9. Je, hajui watakapofufuliwa waliomo makaburini | اَفَلَا يَعْلَمُ اِذَا بُعْثِرَ مَا فِى الْقُبُوْرِ ⑨ |
| 10. Na yatakapodhihirishwa yaliyomo vifuani | وَحُصِّلَ مَا فِى الصُّدُوْرِ ⑩ |
| 11. Kuwa Mola wao Atawajua sana Siku hiyo (viumbe vyake vyote). | اِنَّ رَبَّهُمْ بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيْرٌ ⑪ |

---

1. Mapendeleo ya hakika katika Aya hizi ni kuwa Mwenyezi Mungu anaapa kwa jeshi lililo na farasi wa namna hii; na muradi wake ni kuapa kwa jeshi lenye kushinda katika vita. Kwani hapana shaka kuwa jeshi lililo na farasi namna hii, ni lenye kushinda tu.

Wamirzai hawakusema kweli waliposema kuwa kabla ya Uislamu Waarabu walikuwa hawatumii farasi. Haya ni katika hizo farumu zao za kutaka kuifanya kubwa hiyo tafsiri yao.

6. Muradi wa "kumkanusha Mwenyezi Mungu," ni kukanusha neema zake. Na kukanusha neema ni kutozitumia katika ibada na mambo ya kheri.

7. Yaani: na yeye mwanaadamu anayajua hayo ayatendayo.

8. Au: Ana kuendelea mno katika kupenda mali; nako ni kufanya pupa katika kuyatafuta, na ukiyapata ukayafanyia ubakhili, na ukayaona ndiyo bora kuliko kila kitu.

9-10. Yaani: hajui mwanaadamu kama atakwendalipwa kwa hayo ayatendayo wakati "watakapofufuliwa waliomo makaburini, na yakadhihirishwa na yaliyo vifuani"? Maana Siku hiyo ni ya Kiama.

11. Kujua sana, maana ni Mjuzi wa dogo na kubwa, na lililo wazi na lililofichikana. Siku hiyo atawalipa kwa kila walilolitenda.

آياتها ١١ سورة القارعة مكية (٣٠) (١٠١) ركوعها ١

*Ina Aya 11* — *Ina Kara 1*

# SURAT AL-QARIAH

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. (Msiba) ugongao nyoyo (yaani Kiama)

الْقَارِعَةُ ﴿١﴾

2. (Msiba) ugongao nyoyo ni upi huo?

مَا الْقَارِعَةُ ﴿٢﴾

3. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukaujua) ni upi huo (Msiba) ugongao nyoyo?

وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْقَارِعَةُ ﴿٣﴾

4. Siku ambayo watu watakuwa kama madumadu (watoto wa nzige) waliotawanywa

يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ﴿٤﴾

5. Na milima itakuwa kama sufi zilizochambuliwa (zikawa zinapeperuka).

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ ﴿٥﴾

6. Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito

فَأَمَّا مَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ ﴿٦﴾

7. Huyo atakuwa katika maisha yanayompendeza.

فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَاضِيَةٍ ﴿٧﴾

8. Na yule ambaye mizani yake itakuwa nyepesi

وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ﴿٨﴾

9. Huyo maskani yake yatakuwa katika (huo Moto) — Hawiya.

فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ﴿٩﴾

10. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukaujua) ni nini hiyo (Hawiya)?

وَمَا أَدْرَاكَ مَا هِيَهْ ﴿١٠﴾

11. Ni Moto uwakao kwa ukali (kweli kweli).

نَارٌ حَامِيَةٌ ﴿١١﴾

---

4. Yaani siku hiyo watu watakuwa kama watoto wa nzige katika wingi, na kudangana, na kujitupa huku na huku, hawajui pa kwenda. Na hapo ni watakapoanza kutoka makaburini.

6. Siku hiyo amali zote — nzuri na mbaya — zitapimwa kwa mizani ya Mungu, lakini hatukuambiwa Mizani hiyo itakuwa namna gani. Lakini hapana shaka kuwa Mizani iwezayo kupima hata uzani wa chungu mdogo, na yaliyo katika nyoyo, ni mizani ya Kimungu.

9. Wamirzai wamegeuza makusudi tamko la Umm lililomo katika hii Aya waliyoifanya ya 10; wakasema muradi wa "Ummuhuu" hapa ni mama. Wamefanya hivi ili watie hiyo itikadi yao ya kuwa moto ni mlezi, unaowalea wabaya ili wawe wema. Hii ni tafsiri waliyoizua wenyewe. Ummu hapa ni Makazi, yaani Makazi ya watu wabaya ni Motoni. Tamko la Ummu lina maana mengi, kama ilivyo katika makamusi ya Kiarabu. Katika maana yake ni (a) Mama; (b) Maskani; (c) Mke mkongwe; (d) Mtumishi; (e) Msingi; (f) Mhimili; (g) Raisi . . . Wao wameacha kufasiri kwa Maskani kama walivyofasiri — na wanavyofasiri — wafasiri wote; wameacha hivyo ili watie hiyo farumu yao. Hata katika Kiswahili chetu neno moja huenda likawa na maana mengi; na kila moja ikatumika katika mnasaba wake. Kama (a) Mbuzi: "Nimekuna nazi kwa mbuzi yangu" mbali na "Nimemkama mbuzi wangu." Na (b) Kamba: "Nimekula kamba" na "Nimefunga kamba." Na (c) Buibui: "Kampiga buibui kisha kavaa buibui, akatoka." Na (d) Mkungu: "Alipika wali akaufunika mkungu" na akaula ndani ya mkungu. Na mengi kabisa mengineyo yasiyokuwa haya.

اٰيَاتُهَا ٨ (١٠٢) سُوْرَةُ التَّكَاثُرِ مَكِّيَّةٌ (١٦) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 8* **SURATUT TAKAATHUR** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Kumekughafilisheni kutafuta wingi (wa mali na jaha na watoto na kujifakhirisha kwa hayo)

اَلْهٰكُمُ التَّكَاثُرُ ۝١

2. Hata mumeingia makaburini, (mumekufa kabla ya kufanya kheri yoyote).

حَتّٰى زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ۝٢

3. Sivyo hivyo! Karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo),

كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۝٣

4. Kisha (nasema) Sivyo hivyo! Karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo).

ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُوْنَ ۝٤

5. Sivyo hivyo! Lau kama mnajua ujuzi wa yakini (kuwa sivyo hivyo msingefanya hivyo).

كَلَّا لَوْ تَعْلَمُوْنَ عِلْمَ الْيَقِيْنِ ۝٥

6. Hakika mtauona Moto

لَتَرَوُنَّ الْجَحِيْمَ ۝٦

7. Kisha (nasema:) Mtauona kwa yakini (Moto)

ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِيْنِ ۝٧

8. Kisha kwa hakika mtaulizwa Siku hiyo juu ya neema (mlizopewa mlizitumiaje).

ثُمَّ لَتُسْئَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيْمِ ۝٨ ع

---

1. Ni tabia ya Waarabu — tangu kale — kila kabila kujisifu kwa wingi wa watu na watoto na mali. Basi katika Aya hizi (1-2) Mwenyezi Mungu anawambia: Kufakhiriana kwao kwa wingi, kwa kupenda mno Ulimwengu, kumewashughulisha na kuitumikia Akhera, mpaka yawajilie mauti na wameghafilika nayo.

3. Maana hapo yatakapokujieni mauti mtajuwa kuwa hayo mliyokuwa mkiyafanya siyo.

5. Maana lau kama mnajua yakini kuwa hayo mfanyayo si mazuri, na mnatupa umri wenu bure katika mambo yasiyokuwa na faida yoyote; na yaliyo na faida mumeyawacha, msingeyafanya hayo myafanyayo.

7. Maana hapo mtakapokufa.

8. Mwanaadamu—yeye mzima na kila alicho nacho—ni katika neema za Mwenyezi Mungu. Basi Siku ya Kiama ataulizwa kila neema na namna alivyoitumia.

آياتها ٣ (١٠٣) سُورَةُ الْعَصْرِ مَكِّيَّةٌ (١٣) رُكُوعُهَا ١

*Ina Aya 3*

# SURATUL ASR

*Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Naapa kwa zama (zako ewe Nabii Muhammad)

وَالْعَصْرِ ①

2. Kuwa Binadamu yuko katika hasara

إِنَّ الْإِنسَانَ لَفِي خُسْرٍ ②

3. Isipokuwa wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana (kufuata) haki na wakausiana (kushikamana) na subira (kustahamiliana).

إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ
وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ ③ ع

---

2. Rasilmali ya mwanaadamu katika ulimwengu ni umri wake. Basi kila dakika atakayoitumia mwanaadamu katika mambo ya kheri, ndio faida yake, na kila dakika atakayoitumia katika mambo maovu au yasiyokuwa na haja, ndiyo hasara yake.

3. Katika hao walio "katika hasara" wametolewa wenye kuamini wakatenda vitendo vizuri wakausiana kushikamana na haki na kusubiri. Hawa hawana hasara, sababu akthari ya nyakati zao huzitumia katika mambo ya kuwaletea faida wao na viumbe wenzi wao.

Subira ni namna nne: (a) Kustahamili katika kufanya mambo mema ambayo ni mazito kwa mtu kudumu nayo; na (b) kustahamili katika kuacha mambo maovu ambayo ni mazito kwake kuyawacha; na (c) Kustahamiliana na viumbe wenziwe, awachukulie mabaya yao wala asiwafanyie mabaya yake; na (d) Kustahamili misukosuko ya ulimwengu.

اٰيَاتُهَا ٩ (١٠٤) سُوْرَةُ الْهُمَزَةِ مَكِّيَّةٌ (٣٢) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 9* *Ina Kara 1*

# SURATUL HUMAZAH

*(Imeteremka Makka)*

Kwajina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Adhabu kali itamthubutikia kila mwenye kuramba kishogo, msengenyaji

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةِ ۙ ①

2. Ambaye amekusanya mali na kuyahisabu (tu bila ya kuyatumia katika njia za kheri)

الَّذِىْ جَمَعَ مَالًا وَّعَدَّدَهٗ ۙ ②

3. Anadhani ya kuwa mali yake yatambakisha milele.

يَحْسَبُ اَنَّ مَالَهٗۤ اَخْلَدَهٗ ۚ ③

4. Hasha! Bila shaka atavurumizwa katika (Moto unaoitwa) Hutama.

كَلَّا لَيُنْۢبَذَنَّ فِى الْحُطَمَةِ ۖ ④

5. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) ni nini (Huo moto unaoitwa) Hutama?

وَمَاۤ اَدْرٰىكَ مَا الْحُطَمَةُ ۗ ⑤

6. Ni Moto wa Mwenyezi Mungu uliowashwa (kwa ukali barabara)

نَارُ اللّٰهِ الْمُوْقَدَةُ ۙ ⑥

7. Ambao unapanda nyoyoni.

الَّتِىْ تَطَّلِعُ عَلَى الْاَفْـِٕدَةِ ۗ ⑦

8. Hakika huo (moto) watafungiwa (wawemo ndani yake)

اِنَّهَا عَلَيْهِمْ مُّؤْصَدَةٌ ۙ ⑧

9. Kwa magogo marefu marefu.

فِىْ عَمَدٍ مُّمَدَّدَةٍ ⑨ ع

---

1. Ni kusengenya kwa ishara ulimi ya macho au ya maneno au ya vitendo . . . Na yote ni mabaya. Watu wengi wasahilisha kusengenya, hawaoni kuwa ni kitu. Na katika Qurani yamekuja makemeo makubwa hata kumefananishwa na mtu "Kula nyama ya ndugu yake aliyekufa." Na katika Aya hii Mwenyezi Mungu amesema "*Waylun* . . ." na maana yake ni Adhabu kali. Basi yataka mtu asidharau jambo ovu, khasa lililokemewa katika Qurani.

2. Hii ndiyo hali ya mtu bakhili; ladha yake ni kukusanya mali kisha akiyahisabu kila apatapo faragha. Si kwa haja ya kutaka kujua hisabu yake, la, bali kwa kuona raha tu! Hafikiri kutenda mema ya kumfaa, wala hafikiri kumnufaisha mwenziwe, hatumii yeye mwenyewe, wala hamkubalii mwengine kutumia.

3. Maana: mtu huyo anadhani kuwa hayo mali yake yatamzuilia kufa, abakiye milele katika ulimwengu.

4. Naache kudhani dhana hiyo! Bali atakufa atiwe motoni.

7. Moto huo hautawateketeza nje tu, bali utawateketeza na ndani pia mpaka uunguze hata nyoyo.

8-9. Yaani watafungiwa ndani ya moto kwa magogo marefu marefu ili wasiwe na tamaa ya kutoka tena.

اٰيَاتُهَا ٥ (١٠٥) سُوْرَةُ الْفِيْلِ مَكِّيَّةٌ (١٩) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 5*

## SURATUL FYL

*Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Je! Huoni jinsi Mola wako Alivyowafanya watu wenye ndovu?

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحٰبِ الْفِيْلِ ﴿١﴾

2. Je! Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika

أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِيْ تَضْلِيْلٍ ﴿٢﴾

3. Na akawapelekea ndege makundi kwa makundi

وَّأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيْلَ ﴿٣﴾

4. Wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuchoma

تَرْمِيْهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّنْ سِجِّيْلٍ ﴿٤﴾

5. Akawafanya kama majani yaliyoliwa (yakatapikwa)?

فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُوْلٍ ﴿٥﴾ ع

---

1. Sura hii inaeleza kisa kilichopita karibu ya Makka katika mwaka wa 570 A.C. Yaman siku hizo ilikuwa imetawaliwa na Mahabashi. Nao wakati huo walikuwa Masihia. Liwali wa Yaman aliyekuwa wakati huo ni Abraha. Huyu Abraha alitaka kuwazuilia Waarabu wasende Makka kuzuru Al-Kaaba, akajenga kanisa kubwa akalipamba vizuri katika mji wa S'anaa na akawalazimisha Waarabu wazuru kanisa hilo badili ya Al-Kaaba. Alipokuwa hakufaulu, ndipo alipoazimia kwenda kuivunja Al-Kaaba akakusanya jeshi kubwa na yeye mwenyewe na baadhi ya watu wake wakapanda ndovu. Na kwa sababu hiyo, mwaka ule Waarabu wakawita "Mwaka wa ndovu", au "Mwaka wa wenye ndovu", nao ndio mwaka uliozaliwa Bwana wetu Muhammad (s.a.w.).

Abraha alipofika karibu ya Makka akawapelekea mtu Waarabu kuwapa habari kuwa yeye hakuja kuwapiga wao, bali haja yake ataka wampe nafasi ya kuvunja Al-Kaaba!

Wakati huo Waarabu wa Makka hawakuwa na nguvu za kuweza kupigana wala hawakuwa na mfalme, lakini walikuwa na mkubwa wao akiitwa Abdul-Muttalib, babu yake Bwana wetu Muhammad (s.a.w.) Abdul-Muttalib akawapa amri jamaa zake wote watoke mjini wende majabalini na yeye mwenyewe akaingia katika Al-Kaaba, akamuomba Mwenyezi Mungu ainusuru nyumba yake tukufu, kisha akenda huko waliko kwenda jamaa zake, kumtazama huyo atakayejaribu kuteta na Mungu na kumvunjia nyumba Yake.

Abraha, baada ya kujua kuwa Waarabu wamekwisha jitenga, akajiweka tayari kuingia Makka na kuvunja Al-Kaaba. Papo hapo Mwenyezi Mungu akamletea jeshi Yake (kama utakavyo ona katika Aya ya 3) jeshi ya Abraha ikaingiliwa na maradhi, wengine wakafa papo hapo na Abraha na baadhi ya askari wake wakawahi kurudi Yaman wakafia huko.

3. Wanavyuoni wengine wamesema kwamba inamkinika kuwa makusudio ya "Tair" katika Aya hii ni "viini vya ugonjwa" (germs).

5. Wanavyuoni wengine wamesema kwamba mapendeleo yake ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwatia maradhi mabaya, yakaharibu miili yao, hata wakawa kama majani yaliyoliwa-liwa na wadudu au yaliyoliwa yakatemwa.

اٰيَاتُهَا ٤ (١٠٦) سُوْرَةُ قُرَيْشٍ مَكِّيَّةٌ (٢٩) رُكُوْعُهَا ١

Ina Aya 4

## SURATU QURAYSH
*(Imeteremka Makka)*

Ina Kara 1

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Ili Kuwafanya Makureshi waendelee

لِاِيْلٰفِ قُرَيْشٍ ۝١

2. Waendelee na safari zao za wakati wa kusi (kwenda Yaman) na wakati wa kaskazi (kwenda Shamu, ndiyo maana tukajaalia jeshi la ndovu kushindwa).

اٖلٰفِهِمْ رِحْلَةَ الشِّتَآءِ وَالصَّيْفِ ۝٢

3. Basi nawamuabudu Bwana wa nyumba hii (Al-Kaaba)

فَلْيَعْبُدُوْا رَبَّ هٰذَا الْبَيْتِ ۝٣

4. Ambaye anawalisha (wakati Waarabu wenziwao wamo), katika njaa, na Anawapa amani (wakati wenziwao wamo) katika khofu.

الَّذِيْٓ اَطْعَمَهُمْ مِّنْ جُوْعٍ ۙ وَّاٰمَنَهُمْ مِّنْ خَوْفٍ ۝٤ ع

---

1-4. Al-Kaaba, kama ijulikanavyo, ilikuwa ni mahali patukufu kwa Waarabu wote tangu zama za Sayyidna Ibrahimu (a.s.) ambaye ndiye aliyeijenga kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na kwa kuwa Makureshi ndio waliokuwa walinzi wa nyumba hii tukufu, Waarabu wa makabila mengine wote walikuwa wakiwahishimu na kuwatukuza. Na kwa sababu hiyo waliweza kusafiri wakenda Shamu, katika siku za kaskazi na Yaman katika siku za kusi kwa ajili ya kufanya biashara; na wakirudi kwa salama na amani, pasi na kuchelea kutaaradhiwa na Mabedui njiani na kuuliwa na kupokonywa mali yao, kama walivyokuwa wakifanyiwa Waarabu wengine. Na kilipozuka kisa cha ndovu wakazidi kuhishimiwa na kutukuzwa. Basi katika Sura hii Mwenyezi Mungu anawakumbusha neema hiyo, anawaambia: Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewasahilishia Makureshi kusafiri katika kusi na kasikazi, ili wafanye biashara wapate chakula na mengineyo, akawasalimisha na khofu za njiani zinazowapata Waarabu wengine. Na yote haya ni kwa sababu ya Al-Kaaba, basi nawamuabudu Huyo Mwenye Nyumba hiyo (Al-Kaaba), Aliyewalisha, wasiwe katika njaa, akawasalimisha na khofu. Kwani lau kama si hii Nyumba Yake, wasingeweza kusafiri kwa salama, wala asingekuja mtu katika mji wao, sababu hauna ki...

آياتها ٧ (١٠٧) سورة الماعون مكية (١٧) ركوعها ١

*Ina Aya 7* **SURATUL MAUN** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Je, umemuona (unamjua) yule anayekadhibisha dini, (asiyeamini malipo ya Akhera)?

أرأيت الذي يكذب بالدين ①

2. Huyo ni yule anayemsukuma yatima

فذلك الذي يدع اليتيم ②

3. Wala hajihimizi kuwalisha maskini (wala hawahimizi wenziwe).

ولا يحض على طعام المسكين ③

4. Basi adhabu itawathubutikia wanaosali

فويل للمصلين ④

5. Ambao wanapuuza (maamrisho ya) Sala zao, (kama kuwafanyia wema viumbe wenzao)

الذين هم عن صلاتهم ساهون ⑤

6. Ambao hufanya (amali zao ili watu wawaone tu) riyaa

الذين هم يراءون ⑥

7. Nao hunyima misaada. (Basi Sala zao hazina faida kubwa nao).

ويمنعون الماعون ⑦ ع

---

1. Sura hii inaeleza hali waliyo nayo ghalibu ya watu; hata hao wanaojita Waislamu; nayo ni alama ya wasioamini malipo ya Akhera. Hawawi na huruma kwa wanaadamu wenzao, la kwa kutoa chao wakiwa nacho, wala kwa kuwashakiza wenzao ikiwa wao hawana. Wala hawafanyi jambo jema ila kwa kutaka kusifiwa na watu, na hujizuilia na kufanya ihsani ikiwa haitamvutia manufaa anayoyataraji.

5. Au muradi wake wanapuuza Sala. Nayo ni kusali, na moyo ukawa hauko katika Sala, umeshughulika na mawazo mengine, au kusali kwa riyaa.

6. "Riyaa" ni kufanya amali njema kwa makusudio ya kuonesha watu, ili uonekane kuwa ni mwema kuliko ulivyo, ama upate kupendekeza au upate kilicho mifukoni mwa wenzio. Na hii, kama ambavyo ni namna ya "shirki", kadhalika ni namna ya "wizi".

آياتها ٣ (١٠٨) سُورَةُ الكَوْثَرِ مَكِّيَّة (١٥) ركوعها ١

*Ina Aya 3*

# SURATUL KAWTHAR

*Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١﴾

1. Hakika Tumekupa kheri nyingi.

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ ﴿٢﴾

2. Basi sali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako). (Na kila utakalolifanya lifanye kwa ajili ya Mola wako, siyo mizimu wala mapango wala makaburi).

إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾ ع

3. Hakika adui yako ndiye atakayekuwa mkiwa, (atakatika na kila kheri).

---

1. Makusudio ya "kheri nyingi" hapa ni Utume, ilimu, amali, jaha, kushinda, kupata wafuasi, na kheri nyingine za dunia na Akhera zisizohisabika, ambazo hakupewa mtu kabla yake wala baada yake. Na kheri hizi, hapana shaka ni bora kuliko kheri za mali na watoto.

2. Maana sali kwa ajili ya Mola Wako peke Yake, usiwe kama wale wanaofanya ibada kwa riyaa, na uchinje nyama (wanyama) zako uwape maskini na wenye haja, usiwe kama wale wawafukuzao mayatima na kujizulia na kuwafanyia ihsani wenzao.

3. Maana yake huyo asemae kuwa wewe umetindikiwa na kheri ndiye aliyetindikiwa na kheri siyo wewe. Kheri ulizopewa wewe zitakufaa, na kheri alizopewa yeye za mali na watoto, hazitamfaa kitu.

Maadui wa Mtume (s.a.w.) walikuwa wakifurahi sana kwa kumuona Mtume amefiliwa na watoto wake wanaume, sababu walikuwa wakiona hapana kheri kubwa katika Ulimwengu kama kupewa mali na watoto wanaume. Na kwa sababu hii wakimwita Mtume *Abtar,* Mwenye kukatika na kheri. Basi katika Sura hii Mwenyezi Mungu anamliwaza Mtume Wake, pamoja na kuwajibu wale maadui.

اٰيَاتُهَا ٦ (١٠٩) سُوْرَةُ الْكٰفِرُوْنَ مَكِّيَّةٌ (١٨) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 6* — *Ina Kara 1*

# SURATUL KAFIRUN

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo. — بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Sema: Enyi makafiri. — قُلْ يٰٓاَيُّهَا الْكٰفِرُوْنَ ۝١

2. Siabudu mnachoabudu. — لَآ اَعْبُدُ مَا تَعْبُدُوْنَ ۝٢

3. Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu. — وَلَآ اَنْتُمْ عٰبِدُوْنَ مَآ اَعْبُدُ ۝٣

4. Wala sitaabudu mnachoabudu. — وَلَآ اَنَا عَابِدٌ مَّا عَبَدْتُّمْ ۝٤

5. Wala nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu. — وَلَآ اَنْتُمْ عٰبِدُوْنَ مَآ اَعْبُدُ ۝٥

6. Nyinyi mna dini yenu nami nina dini yangu. — لَكُمْ دِيْنُكُمْ وَلِيَ دِيْنِ ۝٦

---

1. Makafiri wa Makka walipojiona wamechoka, hawawezi kuzima nuru ya Uislamu, na wakamuona Mtume (s.a.w.) kila siku anazidi hima katika kazi yake, na dini kila siku inaendelea mbele, walimwendea Mtume wakamtaka watangamane naye katika ibada, wao wamuabudu Mwenyezi Mungu mwaka mmoja pamoja naye, na yeye atangamane nao katika kuabudu miungu yao mwaka mmoja vile vile; yaani mwaka mmoja waabudu Mungu wote na mwaka mmoja waabudu masanamu pia wote! Ndipo iliposhuka Sura hii.

Na makusudio yake ni haya: Nyinyi muna waungu wenu na namna ya ibada zenu muabudiazo, na mimi nina Mungu Wangu na namna ya ibada nimuabudiayo. Haiwezekani kutangamanisha baina ya Mungu Wangu wa kweli na miungu yenu ya uwongo, wala baina ya ibada yangu ya haki na ibada zenu za batili. Nyinyi muna dini yenu na itikadi yenu; nami nina dini yangu na itikadi yangu.

آياتها ٣ (١١٠) سورة النصر مدنية (١١٤) ركوعها ١

*Ina Aya 3*

## SURATUN NASR

*(Imeteremka Madina)*

*Ina Kara 1*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Itakapofika nusura ya Mwenyezi Mungu na kushinda

إِذَا جَآءَ نَصْرُ اللهِ وَالْفَتْحُ ①

2. Na ukawaona watu wakiingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi

وَرَاَيْتَ النَّاسَ يَدْخُلُوْنَ فِيْ دِيْنِ اللهِ أَفْوَاجًا ②

3. Basi hapo mtakase Mola wako pamoja na kumsifu, umuombe maghufira (msamaha); hakika Yeye ndiye Apokeaye toba.

فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَاسْتَغْفِرْهُ إِنَّهُ كَانَ تَوَّابًا ③ ع

---

1. Huu ni waadi wa Mwenyezi Mungu kumpa Mtume Wake, kuwa atamsaidia amnusuru juu ya maadui zake ambao walikuwa wakimtaabisha na kutaka kumuua, na autawale mji wao waliomtoa; na alipotaka kuingia kwa ajili ya Ibada pia wakamzuilia.

2. Mtume alipoingia Makka na kuwashinda maadui zake, kama alivyoahidiwa na Mwenyezi Mungu, makafiri walikuwa wakija Madina mbele yake, makabila kwa makabila wakiingia katika Dini ya Kiislamu.

3. Maana ya kuambiwa Mtume (s.a.w.) kwamba yatakapofanyika hayo aliyoahidiwa amtakase Mola wake na aombe maghufira; pamoja na kuwa yeye alikuwa akifanya hayo kabla ya hapo, ni kuwa yatakapofanyika hayo aliyoahidiwa, ajali yake Mtume itakuwa imekurubia kwisha. Kwa hivyo anaamrishwa azidishe ibada ili azidi kutengeza Akhera yake.

Hii ndiyo Sura ya mwisho iliyoshuka katika Qurani. Na iliposhuka, baadhi ya Masahaba walifahamu undani wake, wakalia kwa kuona kuwa Mtume anaondoka. Baada ya kushuka Sura hii Mtume (s.a.w.) aliishi siku chache tu.

سُورَةُ اللَّهَبِ مَكِّيَّةٌ (١١١) آياتها ٥ ركوعها (٦)

*Ina Aya 5* *Ina Kara 1*

## SURATUL LAHAB

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ①

1. Pana kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab! Naye amekwisha angamia.

مَا أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ ②

2. Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma.

سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ③

3. (Atakapokufa) atauingia Moto wenye mwako (mkubwa kabisa)

وَامْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ ④

4. Na mkewe, mchukuzi wa kuni (za fitina), (fattani, anayefitinisha watu wasiingie katika dini; atauingia naye Moto huo)

فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍ ⑤

5. (Kama kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayochukulia kuni za fitina hizo).

---

1. Mwanzo wa kupewa Utume Bwana wetu Muhammad (s.a.w.) aliamrishwa awabashirie jamaa zake walio karibu naye kwa kizazi; akawakusanya akawabashiria na kuwakhofisha na adhabu ya Akhera, Abu-Lahab, ami yake, akakasirika, akamwambia 'Mwana kuangamia wee! Ndilo ulilotwitia hili?' Ndipo iliposhuka sura hii kuapizwa Abu-Lahab na mke wake, Ummu-Jamil, aliyekuwa akijipinda sana katika kumuudhi Mtume, na kuwashakiza makafiri wamuue na kufanya kila aliwezalo katika kuizuilia dini isifuatwe.

"Yana kuangamia mikono miwili ya Abu-Lahab!" ni maapizo ya kuapizwa Abu-Lahabi aangamie yeye, badali ya Mtume (s.a.w.). Na alipokuwa Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuapiza, imekuwa hapana shaka maapizo hayo ni yenye kumpata, na kwa hivyo Mwenyezi Mungu anatupa habari kuwa "amekwishaangamia."

5. Huyu mke wa Abu-Lahab alikuwa fattani (sakubimbi). Kazi yake kuchukua maneno ya huku akipeleka huku kwa kutaka kutia fitina na fisadi. Na mtu namna hii Waarabu humshabihisha na "mchukuzi wa kuni." Na dasturi, mchukuzi wa kuni huwa na "kamba" katika shingo yake ya kufungia hizo kuni zake, na kuni ndizo zinazowasha moto. Na huyu mwanamke akiwasha moto wa kuwazuilia watu wasisilimu na kuwatoa waliosilimu.

آياتها ٤ (١١٢) سُورَةُ الإِخْلَاصِ مَكِّيَّةٌ (٢٢) ركوعها ١

*Ina Aya 4*

## SURATUL IKHLAS

*(Imeteremka Makka)*

*Ina Kara 1*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

1. Sema: Yeye ni Mwenyezi Mungu Mmoja (tu).

قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ①

2. Mwenyezi Mungu (tu) ndiye anayestahiki kukusudiwa (na viumbe Vyake vyote kwa kumuabudu na kumuomba na kumtegemea).

اللَّهُ الصَّمَدُ ②

3. Hakuzaa wala Hakuzaliwa

لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ③

4. Wala hana anayefanana Naye hata mmoja.

وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ④

---

1. Baadhi ya makafiri walimtaka Mtume (s.a.w.) awasifie Mwenyezi Mungu, ikashuka Sura hii ya kumtakasa Mwenyezi Mungu na kila namna ya shirki.

"Shirki" ni namna nne: (a) Ni shirki ya kuitakidi kuwa Mungu ni zaidi ya Mmoja, kama walivyokuwa makafiri wa Makka; (b) Ni shirki ya kuitakidi kuwa yuko mwenye uweza wa kufanya jambo ambalo kwa hakika hakuna aliwezaye ila Mwenyezi Mungu, kama kunyesha mvua na kuondoa balaa, na mengineo katika mambo ambayo yametoka katika uweza wa viumbe. Na shirki ya namna hii imeingia kwa baadhi ya wajitao "Islamu" siku hizi, Mungu Atunusuru; (c) Ni shirki ya kuitakidi kwamba Mwenyezi Mungu ana fungamano baina Yake na viumbe vyake, kama waitakidivyo Wamasihia; (d) Ni shirki ya kuitakidi kwamba Mwenyezi Mungu ana mfano katika Dhati Yake au Sifa Zake, kama waitakidivyo Mayahudi na wengineo. Basi Sura hii imekanusha, na imemtakasa Mwenyezi Mungu na namna zote hizo.

(١١٣) سُورَةُ الْفَلَقِ مَكِّيَّة (٢٠) آيَاتُهَا ٥ رُكُوعُهَا ١

*Ina Aya 5* **SURATUL FALAQ** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.**

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ ①

1. Sema: Ninajikinga kwa Mola wa ulimwengu wote

مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ②

2. Na shari ya Alivyoviumba

وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ③

3. Na shari ya giza la usiku liingiapo

وَمِن شَرِّ النَّفَّاثَاتِ فِي الْعُقَدِ ④

4. Na shari ya wale wanaopulizia (vivia) mafundoni, (wakavunja mashikamano yaliyo baina ya watu, yaani shari ya mafatani)

وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ⑤

5. Na shari ya hasidi anapohusudu.

---

1. Sura hii na iliyo baada yake zimeshuka pamoja na iko khitilafu kuwa zimeshuka Makka au Madina. Na zote Sura mbili zatufunza namna ya kujitia katika "Himaya" ya Mwenyezi Mungu, na kutufahamisha kwamba Yeye ndiye Mwenye Uweza wa kumlinda mtu na kila jambo, sababu Yeye ndiye Mwenye kuumba kila kitu. Basi mwenye kuwacha kujitia katika "Himaya" Yake, akajitia katika Himaya ya mchawi au mzimu au kaburi, atakuwa amejitia katika namna ya shirki (b) tuliyoitaja katika maelezo ya Sura iliyopita.

2. Katika "alivyoviumba" anaingia kila kiumbe, mwenye roho na asiyekuwa na roho, aonekanaye na asiyeonekana.

3. Hapana shaka kuwa usiku wa kiza una balaa nyingi ambazo hazipatikani mchana wala katika usiku wa mwezi, kama nyama waovu, wevi, mashetani (wanaowaamrisha watu kufuata mabuibui yapitayo) na balaa nyenginezo tuzijuazo na tusizozijua, ambazo hujificha kukiwa na muangaza na kudhihiria kukiwa na kiza.

5. "Hasidi" ni mtu ambaye huchukiwa kwa kumuona mwenziwe ameneemeshwa na Mwenyezi Mungu, na kutamani imuondokee neema ile, japo asiipate yeye. Nayo ni katika maasia makubwa, na maradhi mabaya kabisa! Na hasidi pengine huficha ile hasadi yake katika moyo mpaka akajifia, akapumzika yeye, na watu wakapumzika na utesi wake usiokuwa na sababu. Na pengine huwa hatosheki kwa kuweka moyoni, bali hufanya na kila aliwezalo ili kumuondolea mwenziwe hiyo neema aliyoneemeshwa na Mwenyezi Mungu, hata kwa kutoa chake bali na hata kwa kumuua yule mwenziwe, ikiwa hapana budi. Na hasadi ya namna hii ni mbaya zaidi.

اٰيَاتُهَا ٦ سُوْرَةُ النَّاسِ مَكِّيَّةٌ (٢١) (١١٤) رُكُوْعُهَا ١

*Ina Aya 6* **SURATUN NAAS** *Ina Kara 1*

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Sema: Ninajikinga kwa Bwana Mwenye kuwalea

قُلْ اَعُوْذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۙ ﴿١﴾

2. Mfalme wa watu

مَلِكِ النَّاسِ ۙ ﴿٢﴾

3. Muabudiwa wa watu

اِلٰهِ النَّاسِ ۙ ﴿٣﴾

4. Na shari ya mwenye kutia wasiwasi mwenye kurejea nyuma

مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ ۙ الْخَنَّاسِ ۙ ﴿٤﴾

5. Atiaye wasiwasi nyoyoni mwa watu

الَّذِىْ يُوَسْوِسُ فِىْ صُدُوْرِ النَّاسِ ۙ ﴿٥﴾

6. (Ambayc ni) katika majini na watu.

مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ﴿٦﴾ ع

1. Mwenyezi Mungu baada ya kuwa ni Bwana wa watu kadhalika ndiye mwenye kuwalea tangu walimatumboni hata wakamaliza umri wao katika ulimwengu, kwa roho na kiwiliwili na pumzi na chakula na maji na kila wahitajialo katika maisha yao, kisha akawapa akili, akawaonesha njia ya "kheri" ya dunia na Akhera, akawaamrisha waifuwate; akawaonesha na njia ya "shari" ya dunia na Akhera, akawaamrisha waiepuke na watahadhari nayo.

4. "Mwenye kutia wasiwasi, mwenye kurejea nyuma"; ni Sheitani, ambaye kazi yake ni "kutia wasiwasi katika nyoyo za watu" akawapoteza. Lakini wakati akipambana na wenye Imani ya nguvu, au mwenye kuzinduka akakumbuka Mola Wake, shetani hushindwa, akarejea nyuma.

6. Katika lugha ya Kiarabu kila muovu hufaa kuitwa "Sheitani" ni sawa alikuwa katika Majini, wanaadamu au nyama. Na "Shetani" wa kibinadamu huwa muovu zaidi kwa mwanaadamu mwenziwe kuliko masheitani.

PRINTED IN INDIA

# دعاء ختم القرآن

صدق الله العلي العظيم ○ وصدق رسوله النبي الكريم ○ ونحن على ذلك من الشاهدين ○
ربنا تقبل منا إنك أنت السميع العليم ○ اللهم ارزقنا بكل حرف من القرآن حلاوة و
بكل جزء من القرآن جزاء ۔ اللهم ارزقنا بالألف ألفة وبالباء بركة وبالتاء توبة وبالثاء ثوابا
وبالجيم جمالا وبالحاء حكمة وبالخاء خيرا وبالدال دليلا وبالذال ذكاء وبالراء رحمة وبالزاء
زكوة وبالسين سعادة وبالشين شفاء وبالصاد صدقا وبالضاد ضياء وبالطاء طراوة
وبالظاء ظفرا وبالعين علما وبالغين غنى وبالفاء فلاحا وبالقاف قربة وبالكاف
كرامة وباللام لطفا وبالميم موعظة وبالنون نورا وبالواو وصلة وبالهاء هداية
وبالياء يقينا ۔ اللهم انفعنا بالقرآن العظيم ○ وارفعنا بالآيات والذكر الحكيم ○ وتقبل
منا قراءتنا وتجاوز عنا ما كان في تلاوة القرآن من خطاء أو نسيان أو تحريف كلمة
عن مواضعها أو تقديم أو تأخير أو زيادة أو نقصان أو تأويل على غير ما أنزلته
عليه أو ريب أو شك أو سهو أو سوء ألحان أو تعجيل عند تلاوة القرآن أو كسل أو
سرعة أو زيغ لسان أو وقف بغير وقوف أو إدغام بغير مدغم أو إظهار بغير بيان أو
مد أو تشديد أو همزة أو جزم أو إعراب بغير ما كتبه أو قلة رغبة ورهبة عند
آيات الرحمة وآيات العذاب فاغفر لنا ربنا واكتبنا مع الشاهدين ○ اللهم نور قلوبنا
بالقرآن وزين أخلاقنا بالقرآن ونجنا من النار بالقرآن وأدخلنا في الجنة بالقرآن
اللهم اجعل القرآن لنا في الدنيا قرينا وفي القبر مونسا وعلى الصراط نورا وفي الجنة
رفيقا ومن النار سترا وحجابا وإلى الخيرات كلها دليلا واكتبنا على التمام وارزقنا
أداء بالقلب واللسان وحب الخير والسعادة والبشارة من الإيمان ○ وصلى الله
تعالى على خير خلقه محمد مظهر لطفه ونور عرشه سيدنا محمد وآله وأصحابه
أجمعين وسلم تسليما كثيرا كثيرا ○